SUPA JACKPOT
TZS.1,159,574,731
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#


Nipashe
Ijumaa Oktoba 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581455
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 4
**Watendaji** h'shauri wabainika hujuma uboreshaji shule

UKURASA WA 17
**Wakazi** Uwanja wa Ndege Pemba kulipwa fidia



UKURASA WA 19
**Chongolo** ataka kasi mradi ujenzi wa mabwawa





# Zahanati zilizokamilika miaka minne hazitumiki

• **Mganga** Mkuu: Shida watumishi, vifaa... *Endelea ukurasa 3*





Mwonekano wa jengo la zahanati ya Isulilo, kata Busangi, wilayani Maswa mkoani Simiyu jana, lililokamilika kwa zaidi ya miaka minne bila ya kuanza kutoa hudumu kwa wananchi. Picha ndogo: Vitasa vya milango vikiwa vimeharibika na dawa zikiwa zimetelekezwa. **PICHA: ALEX SAYI**

## Kelele za jenereta, vipaza sauti, joto mtihani Kariakoo

UKURASA 2



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga, akiwaonyesha waandishi wa habari jana, dawa za kulevya aina ya bangi zilizotengenezwa kwa mfumo wa biskuti, baada ya kuwakamata watu wanne kwa tuhuma za kuzisafirisha. Habari zaidi **Uk. 16.** **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Ongezeko wagonjwa wa akili lashtua

UKURASA 5

**MICHEZO** GAMONDI AWATAJA HAWAKUWA MAKINI UK.24
**KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akikabidhi cheti kwa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Care International Tanzania, Prudence Masako kwa kutambua mchango wa shirika hilo kwa kusaidia Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) za nchini, wakati wa mkutano wa jukwaa la mwaka la mashirika hayo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kelele za majenereta, vipazasauti na joto balaa umeme wa ratiba Kariakoo

**Na Jenifer Gilla**

KWA sasa viunga vya biashara ndani ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam vinatawaliwa na kelele za majenereta, vipazasauti vya biashara vinavyoshindana kwenye vichochoro vya biashara kila umeme unapokatika, Nipashe imeshuhudia.

Hiyo ndio picha halisi ya 'mkoa' huo wa biashara pale huduma hiyo inapokosekana, huku wenyeji wa biashara hiyo wakifafanua kuwa kwa waliomo katika maduka ya uvunguni, shida ya joto na giza iko katika orodha ya magumu.

Kwa mujibu wa mfanyabiashara wa vitambaa katika Mtaa wa Narung'ombe na Ndanda, Awadh Said, ni hali inayowaathiri zaidi kiafya, pia kukumbana na wizi katika eneo hilo lenye kundi kubwa la watu.

Alimwambia mwandishi wa habari hizi jana kuwa analazimika kwenda nje ya duka lake umeme unapokatika kutokana na joto kuwa kali, ili kujiepusha na madhara ya kiafya anayokumbana nayo mara kwa mara joto linapozidi.

"Mimi mwenye presha, joto likizidi nalo si zuri. Kwahiyo, kama hivi umeme ukikatika ninatoka nje, ili nipate hewa vinginevyo watanibeba wanirudishe nyumbani," alisema.

Mfanyabiashara Happy Ernest katika Mtaa wa Narung'ombe na Msimbazi, eneo lililozibwa na biashara mbalimbali, alilalamika kwamba umeme unapokatika wanakumbana na kelele zilizopitiliza kutoka kwenye majenereta na vipazasauti ambavyo ni vikwazo kwenye biashara zao.

Alisema kelele hizo zinakuwa kubwa kiasi cha kutoelewana vizuri na wateja wao, kushindwa kupokea simu za oda kutoka kwa wateja wa mbali, hali inayochangia wakati mwingine kupeleka oda tofauti kwa mhusika.

Mfanyabiashara wa viatu vya plastiki katika mtaa huo, Japhet Mushi, alimweleza mwandishi kuwa umeme unapokatika wanapata hasara kwa kuwa watu wasio waaminifu wanatumia nafasi hiyo kwenda kuwaibia kutokana na kuwapo giza.

Alisema ni rahisi watu hao kuiba bidhaa kwa kuwa maduka hayo ni madogo na bidhaa ni nyingi, hali inayowalazimu kuweka baadhi kwenye korido ambayo watu wa aina mbalimbali wanapita, hivyo si rahisi kumwona mteja akichukua bidhaa umeme unapokuwa umekatwa.

"Kama unavyoona hapa bidhaa zimejaa korido nzima, hata watu kupita tu ni shida. Kwahali kama hii umeme unapokuwa umekatika, mtu akiokota kiatu si rahisi kumwona. Sasa kuna wezi wamejiandaa kabisa umeme ukikatika tu wanakuja kuiba, unashangaa tu boksi limepungua bidhaa," alisimulia kwa uchungu Japhet.

Alisema ni kawaida kwake kuibiwa pea tatu hadi tano za viatu vya plastiki, maarufu yeboyebo, pale umeme unapokatika kutokana na ufinyu wa eneo analofanyia biashara kumzuia kuona kwa umakini wateja wake.

Alisema katika kukabiliana na hali hiyo, walikaa kikao na wafanyabisahara na kukubaliana kuchanga fedha ili kununua jenereta, lakini bado suala hilo halijakamilika na kuomba serikali kutowafikishia mgawo ili kuwaepusha na hasara hizo.

Mfanyabisahara wa nguo za kike katika Mtaa wa Msimbazi, Nancy Jacob, aliishukuru serikali kwa kutoliweka soko hilo kwenye mgawo wa umeme kwa sasa akiamini imeona umuhimu wa eneo hilo kuwa na huduma hiyo muda wote.

"Tangu mgawo uanze hapa dukani kwangu haujawahi kukatika. Ninaishukuru TANESCO na serikali kwa kutufikiria na kuona umuhimu wa sisi kuendelea kupata nishati hii kwa sasa, tunawaomba waendelee kutuangalia hata siku za mbele," alisema.

Wiki iliyopita Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilibainisha kuwapo na upungufu wa uzalishaji umeme unaotokana na upungufu wa maji katika mito na mabwawa.

Lilisema hali hiyo imeathiri uzalishaji umeme katika vituo vya kuzalisha umeme vinavyotumia maji, athari kubwa zikitokea katika vituo vya Kihans, Kidatu na Pangani.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa umeme Oktoba 2 mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Gissima Nyamo-Hanga, alisema kuna upungufu wa megawati 300 hadi 350 kutoka 400 za wiki moja nyuma.

Alisema TANESCO ilifanya kazi kubwa ya kutengeneza mitambo na kupata gesi kwa ajili kuzalisha umeme zaidi ili kuondokana na upungufu wa megawati 400 katika Gridi ya Taifa, hali iliyochangia kupunguza makali ya umeme wa ratiba.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alilielekeza shirika hilo kuharakisha urekebishaji mitambo kwa wakati, ili kuimarisha upatikanaji umeme kwa kuwa uzalishaji ukiwa mdogo wakati mahitaji ni makubwa, upungufu wa umeme unatokea.

Pia aliliagiza shirika hilo kufanyia kazi kwa haraka hitilafu zote zilizotokea, ili umeme uendelee kupatikana na kuboresha kitengo cha huduma kwa wateja ili Watanzania wanapopata hitilafu ndogo za umeme wazitatue kwa wakati.

# Mpango azishushia rungu NGO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameelekeza mambo manne kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, ikiwamo kutokubali kuwa matarumbeta ya watu wasioitakia mema Tanzania.

Wakati akitoa maagizo hayo, Dk. Mpango ameitaka Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kufanya uchambuzi wa kina wa mwenendo wa mashirika hayo na kuishauri serikali.

Akizungumza jana kwenye jukwaa la mwaka la NGO, Dk. Mpango alisema; "Mashirika yetu yasiyo ya kiserikali hapa nchini ninawaomba sana msikubali kutumiwa. Maadili yetu ni mazuri ya Kitanzania lazima tuyatunze na tuyalinde. Msikubali kuwa matarumbeta ya watu wasiotutakia mema."

Alisema, NGO zinawajibika kutunza na kulinda maadili kwa kuheshimu mila, desturi za kitanzania katika utekelezaji wa afua na program mbalimbali.

"Niwakumbushe kuzingatia sheria za nchi kufuata miongozo mbalimbali inayoratibu shughuli za mashirika yenu. Wizara ya Maendeleo ya Jamii ninaiomba ishirikiane na wadau wengine katika kusimamia hili.

"Hili ni muhimu sana Tanzania ni ya kwetu na watu wasitumie mlango wa mashirika yasiyo ya kiserikali kupenyeza ajenda zao ambazo haziendani na maadili ya Kitanzania. Ninaiomba Kamati ya Bunge mfanye uchambuzi makini wa mchango wa mashirika yasiyo ya serikali na kuishauri serikali ipasavyo. Sisi tumefungua masikio kama kawaida tuko tayari kupokea ushauri wa bunge juu ya mwenendo na ufanisi wa mashirika yasiyo ya kiserikali,"alisema.

Pia, aliagiza uwajibikaji na uwazi katika mashirika hayo kwa kuwa bado hakuna uwazi wa kutosha kuhusu rasilimali zinazopatikana na namna yanavyotumika katika kutekeleza miradi iliyokusudiwa na wakati mwingine matumizi ya rasilimali hizo hayawiani na malengo.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi, alisema eneo hilo ni muhimu kuangaliwa na mashirika hayo kwa jicho la kipekee kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinaathiriwa na tatizo hilo.

Alisema, serikali ingependa kuona ushiriki zaidi wa NGO katika kutoa elimu na hamasa kuhusu uhifadhi wa mazingira, udhibiti wa majanga, maisha endelevu, utunzaji wa misitu na uoto wa asili na kuchangia katika utengenezaji na uboreshaji wa sera mbalimbali.

"Mimi naamini mnayo nafasi ya kubuni programu muhimu kama ukusanyaji na urejelezaji wa taka, biashara za kaboni, uanzishaji na utunzaji wa vitalu vya miti pamoja na usafi wa mazingira katika maeneo yetu ikiwamo fukwe za bahari, maziwa," alisema.

Alielekeza serikali ngazi za mikoa na wilaya kufanya kazi kwa karibu na mashirika hayo na kufuatilia kazi zao. Pia, alisema serikali inafahamu viko vikwazo vinavyoathiri ufanisi wa mashirika na kwamba ni vyema kwa pamoja kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

Sambamba na hayo, alitaka mashirika kujitegemea ili kuacha kutegemea fedha za wafadhili ambazo zinapungua mwaka hadi mwaka.


Naye Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema kupitia jukwaa hilo yamejadiliwa masuala mbalimbali ikiwamo namna ya kuongeza ubunifu ili kuchochea ukuaji wa mashirika hayo na kusimamia misingi na uwajibikaji.

Aidha, alisema kuna ramani ya kidigitali ya utambuzi wa mashirika hayo ambayo itasaidia kutambua zilipo, miradi na afua zinazotekelezwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCONGO), Dk. Lilian Badi, alisema mashirika hayo yanakabiliwa na vikwazo mbalimbali ambavyo vinakwamisha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za mashirika hayo nchini.

"Changamoto hizi ni pamoja na ya kupatikana misamaha ya kodi, kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, kuna changamoto ya muda unaotumika kupata vibali kwa ajili ya kutekeleza miradi na afua mbalimbali katika sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa,"alisema.

Pia, alisema mifumo wa ulipaji kodi si rafiki na baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa kutotekeleza sheria na wamekuwa watekelezaji wa moja kwa moja wa miradi na kuyanyima fursa mashirika ya ndani.



# DC aingilia kati mgogoro wa watawa na wananchi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SERIKALI imeingilia kati mgogoro baina ya wananchi wa kijiji cha Mlangoni, Siha mkoani Kilimanjaro na Watawa wa Shirika la Kazi ya Roho Mtakatifu (Holly Spirit Sisters).

Mgogoro huo umedumu kwa muda mrefu na ulikolezwa na tukio la mauaji ya mkazi mmoja wa Kitongoji cha Kilari, Nicholas Nzota.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Christopher Timbuka (pichani), aliingilia kati na kuiomba familia ya Nzota, aliyeuawa kwa kupigwa risasi kichwani na mlinzi wa watawa hao, kuridhia kuuzika mwili wa ndugu yao jana.

Juzi, familia ya Nzota iliweka mgomo ikitoa masharti magumu kutaka yafuatwe ili ikubali kuzika mwili huo.

Akizungumza jana, Dk. Timbuka alisema Watawa wa Shirika la Holly Spirit Sisters-Kilari, wamekubali kubeba gharama za maziko ya Nzota, ambaye aliuawa kwa risasi jioni ya Oktoba Mosi, mwaka huu.

"Kikubwa tulichofanya ni kuwaelimisha ndugu kwamba hili suala limetokea na haiwezekani kurudisha kitu chochote kile nyuma na kwamba ukichukulia kwenye taratibu za mtu aliyeuawa, masista (Watawa) hawakutuma mtu au askari kwamba aue. Wanaposema wanasusia kuzika, wanamsusia nani pale?

"Na ili tumtendee haki marehemu na familia yake, ni vizuri wakakubali kuzika. Kwa hiyo hicho ndicho tulichowaambia ni kikubwa tulichotaka ni kuwa na amani pande zote mbili, yaani upande wa Watawa na upande wa wanakijiji wote.

"Wote wamekubaliana kweli mazingira wanayoyaishi sasa si mazuri na kwamba wako tayari kufanya kikao cha upatanisho. Kwa hiyo, tutakapomaliza mazishi (maziko), tutaandaa kikao cha pande zote sasa kuwapatanisha ili waishi vizuri kama Watanzania. Hata leo (jana) baadaye nitaenda kwenye huo msiba nikiwa na watawa pia, na wamekubali kubeba gharama za maziko ya marehemu," alisema Dk. Timbuka

Oktoba 3, mwaka huu, mdogo wa marehemu Nzota, alisema kifo cha kaka yake kimewaumiza sana na kama familia na hawawezi kuzika mpaka watakapopata mwafaka wa familia yake itakavyoachwa kwa kuwa alikuwa tegemeo.

Chanzo cha mzozo kinachodaiwa kusababisha kifo cha Nzota ni utashi wake wa kujitokeza kuhoji sababu za walinzi wa shirika hilo la watawa kuwashikilia wanawake wawili katika mazingira yenye utata baada ya kusikika wakipiga yowe kuomba msaada.

Juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Yahya Bwanamdogo, alisema wanamshikilia mlinzi huyo (jina limehifadhiwa) kwa ajili ya mahojiano zaidi.

# Zahanati zilizokamilika miaka minne iliyopita hazitoi huduma

## -Mganga Mkuu: Shida watumishi, vifaa

**Na Alex Sayi,** MASWA

BAADHI ya wananchi wilayani Maswa mkoani Simiyu wameeleza kukerwa na kitendo cha kuwapo zahanati mpya mbili zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, lakini hazitumiki kwa miaka minne sasa.

Walibainisha kero hiyo juzi walipozungumza na mwandishi wa habari hizi, wakiwalalamikia baadhi ya watendaji wa serikali na wanasiasa kuendelea kuwapa ahadi kila wanapoitisha mikutano ya hadhara kuwa zhanati hizo ziko mbioni kuanza kutoa huduma.

Walilalamika wanapata shida kupata huduma ya matibabu kwa kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma.

Zahanati hizo ni pamoja na ya Isulilo iliyoko Kata ya Busangi na Zahanati ya Ng'ham iliyoko Kitongoji cha Ng'hami, Kata ya Nyalikungu wilayani hapa.

Zote zimejengwa kwa nguvu za wananchi, wadau wa afya na halmashauri, lakini hazitoa huduma iliyokusudiwa.

Kabula Ng'hungu (45), mzazi wa watoto wanane na mkazi wa Kitongoji cha Ng'hami, Mtaa wa Ilula ambaye pia ni mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) alimwambia mwandishi kuwa licha ya kutoa michango yao ya fedha na nguvu kufanikisha ujenzi wa zahanati hizo, wanashangaa kuona hazitoi huduma kwa madai kuwa huduma ya choo haijakamilika.

"Ujenzi ulianza 2010 na kukamilika mwaka 2020, lakini mpaka sasa sababu tunayopatiwa ni kuwa huduma ya vyoo haijakamilika na nyumba za watumishi hakuna, taarifa ambazo tunashindwa kuzielewa kama wananchi tunaohitaji huduma," alilalama mama huyo.

Alisema kuwa kama wanufaika wa TASAF, walishiriki kuchangia ujenzi huo kwa kiasi cha Sh. 40,000 kila mnufaika mwaka wa fedha 2020/21, fedha zilizokatwa moja kwa moja kutoka katika mgawo wao.

Limi Lugembe (60), mkazi wa kitongoji cha Ng'hami alisema mara kadhaa wajawazito wamekuwa wanajifungulia nyumbani kwa kukosa huduma kutokana na huduma za afya kuwa mbali na maeneo yao, hivyo kuomba serikali kutatua kero hiyo ili waanze kupata huduma kwa karibu.

"Wananchi hadi tumekata tamaa na zahanati hii kila kikao kikiitishwa kinahusu kuchangia. Tumechangia wee.. hatuoni hatima yake. Akija diwani au mbunge wanaishia kutuahidi tu kituo kiko mbioni kutoa huduma ndani ya mwaka huu. Serikali imeshakipangia kituo madaktari lakini kila tukiangalia hatuoni chochote," alidai mama huyo.

Angelina Phaustine (24), mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema: "Kiukweli kinamama tunapata shida mno hasa wakati wa kujifungua. Ninakumbuka nilijisikia uchungu saa saba usiku, mume wangu akamtafuta bodaboda, lakini hadi anafika alikuwa ameshachelewa uchungu ulikuwa umenizidia. Nikalazimika kujifungulia nyumbani."

Mwandishi alifika katika zahanati ya kitongoji hicho na kujionea kinachoendelea; majengo yameanza kuchakaa, baadhi ya milango imeshaliwa na mchwa, rangi imeshachanganyikana na vumbi.

Ni zahanati ambayo ujenzi wake ulianza miaka 13 iliyopita, ukigharimu zaidi ya Sh.milioni 70. Kati yake Mfuko wa Jimbo ukichangia Sh. milioni saba, wadau wa maendeleo Sh. milioni nne, michango ya wananchi na wanufaika wa TASAF Sh. milioni sita na halmashauri Sh. milioni 50.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswenge Kaminyoge akiwa ziarani hivi karibuni katika kata hiyo, pamoja na mambo mengine, aliwelekeza Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Ziza Zegeja kuhakikisha zahanati hizo zinaanza kutoa huduma kwa wananchi mwishoni mwa mwezi uliopita, lakini bado hazijaanza kufanya kazi.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Dk. Zegeja, akizungumzia suala hilo, alisema tayari dawa na vitanda vinne vimeshapelekwa katika Zahanati ya Ng'ham na madaktari wawili wamepangwa kituoni huko tayari kuanza kazi kuanzia mwishoni mwa mwezi uliopita.

Alisema si kwa kituo hicho tu, vituo vyote ambavyo vimekamilika wilayani mwake vimepelekewa dawa na matabibu ili kuanza kutoa hudumu ikiwamo Zahanati ya Njiapanda iliyoko Kata ya Isangi ambayo nayo ilitakiwa kuanza kufanya kazi kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.

**HOJA YA CAG**

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anabainisha kuwapo miradi ya afya iliyokamilika yenye thamani ya Sh. bilioni 4.93 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16 kwa muda wa miezi mitatu hadi miaka mitatu.

Kwa mujibu wa CAG Charles Kichere, miradi hiyo inahusisha zahanati, jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kituo cha afya.

CAG ana angalizo katika hilo kuwa dosari hiyo inasababishwa na ukosefu wa

vifaa tiba, ukosefu wa wafanyakazi na miundombinu rafiki.

Kilichoshuhudiwa na mwandishi wilayani Maswa kinakinzana na Lengo Na. 3 la Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG) linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha afya

njema na ustawi wa watu wa rika zote.

Vilevile, hali hiyo inakinzana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2022/26) unaokusudia kuimarisha mifumo ya usimamizi upatikanaji na utoaji huduma za afya nchini.

Hali hiyo pia ni kinyume cha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2007 unaoelekeza serikali ihakikishe kunakuwa na zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata.


**LEARNIT INSTITUTE OF BUSINESS AND TECHNOLOGY LIMITED**
**HAILE SELASSIE STREET, PLOT NUMBER 14, BLOCK NUMBER 14, HOUSE NUMBER 15, DAR ES SALAAM**
**AT AN EXTRAORDINARY GENERAL MEETING OF THE MEMBERS OF THE COMPANY HELD AT THE REGISTERED OFFICE ON THE 1ST DAY OF OCTOBER, 2023, THE FOLLOWING SPECIAL RESOLUTION WAS DULY PASSED.**

**SPECIAL RESOLUTION:**

1. It was RESOLVED that the Company be wound up voluntarily under sections 334 and 345 of the Companies Act 2002 as proposed by the Members of the Company which took effect from 1ST .day of July 2023.
2. It was RESOLVED that ALLEN KIMBELWA under the care of Adelphos (T) Limited be appointed as liquidator of LEARNIT INSTITUTE OF BUSINESS AND TECHNOLOGY LIMITED for the purpose of winding up the company's affairs and distributing its assets if any.
3. It was RESOLVED that Liquidator published the notice of winding the company voluntarily by the members in the newspapers of Uhuru and Nipashe dated 18th day of August 2023 and Government gazette dated 18th day of August 2023.
4. It was further RESOLVED that Liquidator has furnished the report and final accounts of the company before the members.
5. It was further RESOLVED that all members be informed of this development and the necessary documents to this effect, be prepared, signed, and filed with the Company registry.

IT IS HEREBY CERTIFIED that the above was duly passed in accordance with and complied with the Memorandum and Articles of Association. Dated and signed at Dar es Salaam this .........day of .................. 2023.

.......................................... ..................................
**CHAIRPERSON** **MEMBER**



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Nelson Mlali, akiwasilisha taarifa ya shirika hilo kwa wahariri na waandishi wa habari, jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAC yajivunia makusanyo kwa miaka mitano

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limekusanya zaidi ya Sh. bilioni 43 katika kipindi cha miaka mitano huku likitangaza fursa kwa wananchi kujiajiri katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji nchini.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa TASAC, Nelson Mlali, wakati akizungumza na waandishi wa habari na wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu mafanikio ya shirika hilo kwa kipindi hicho cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2021/22.

Alisema kiasi hicho ambacho ni ongezeko la mchango mkuu wa serikali kilikusanywa katika kipindi hicho kutoka zaidi ya Sh. bilioni 9.1 hadi Sh. bilioni 43. 4.

Mlali alifafanua kuwa shirika hilo ambalo lilianzishwa Februari 23, 2018, lilikusanya Sh. bilioni 9.1 (2018/19), Sh. bilioni 20.1 (2019/20), Sh. bilioni 31.8 (2020/21) na Sh. bilioni 43.4 (2021/22)

Aliyataja mafanikio mengine ambayo TASAC imeyapata kwa kipindi hicho kuwa ni kuongeza idadi ya kadhia zilizohudumiwa kutoka 6,000 hadi kufikia zaidi ya 10,000.

Kuunda nyenzo za udhibiti wa usafiri majini ikiwa ni pamoja na Kanuni na Miongozo ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria katika kudhibiti usafiri majini.

Kuongeza idadi ya watoa huduma wanaodhibitiwa na TASAC kwa maana ya idadi ya leseni na vyeti vya usajili vilivyotolewa, idadi ya vyeti kwa mabaharia waliokidhi masharti kutoka 5,699 hadi 17,689.

Idadi ya leseni za vyombo vidogo kutoka 2,000 hadi 6,366, ukaguzi wa meli za kigeni na mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Vilevile, kuimarisha udhibiti wa huduma za bandari baada ya urasimishaji wa maeneo 20 katika mwambao wa Bahari ya Hindi na maziwa nchini. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mikataba, itifaki na miongozo inayotolewa na Shirika la Bahari Duniani (IMO) na kuridhiwa na serikali.

Kuzuia na kupambana na umwagikaji wa mafuta baharini, kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2018/19 hadi 2020/21.

Pia, kuwa miongoni mwa taasisi 10 bora nchini katika mwaka wa fedha 2020/21 kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Kwa mujibu wa Mlali, mafanikio hayo yamepatikana kutokana na serikali kupokea ushauri wa kitaalam, miongozo na maelekezo sahihi kupitia Wizara ya Uchukuzi na kamati za Bunge na ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya usafiri kwa njia ya maji nchini.

"Shirika linaendelea na utekelezaji wa mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi Ziwa Victoria unaotarajiwa kukamilika Desemba mwakani, ujenzi wa boti tano za uokozi, mbili Ziwa Victoria, nyingine mbili Ziwa Tanganyika na moja Ziwa Nyasa," alisema.

Alizitaja fursa hizo kuwa ni kuanzisha usajili wa meli kwa masharti rafiki, maeneo ya ukarabati na ujenzi wa meli katika Ukanda wa Pwani.

Nyingine ni uanzishwaji wa maegesho ya boti ndogo, viwanda vya utengenezaji malighafi za ujenzi wa boti za plastiki, bandari rasmi za uvuvi na kukidhi mahitaji ya soko la Comoro.

"Sensa ilibaini idadi ya vyombo vidogo vya majini ni 52,189 kati ya vyombo hivyo, vidogo vya majini vyenye urefu wa mita nne na zaidi ni 45,976 sawa na asilimia 88," alisema.

Hata hivyo, alisema TASAC inaendelea kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya haraka ya teknolojia katika sekta na mahitaji makubwa ya mifumo ya TEHAMA na uhaba wa wataalamu wa ndani katika baadhi ya taaluma hasa wakaguzi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini.

Alisema kwa kushirikiana na vyuo na taasisi vinavyotoa mafunzo ya ubaharia kikiwemo Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) wataongeza uwezo na wigo wa kutoa mafunzo na kuzalisha wataalamu wanaohitajika.

## Jela miaka miwili, viboko sita kwa kujifanya wakili

**Na Samson Chacha,** TARIME

MAHAKAMA ya Mwanzo Tarime Mjini mkoani Mara, imemhukumu Jefason Kasera (40), kwenda jela miaka miwili na kuchapwa viboko sita.

Hukumu hiyo imetolewa baada ya Kasera kupatikana na hatia ya kujifanya wakili wa kujitegemea kwa kujitambulisha mbele ya mahakama wakati kesi ya madai ilipokuwa ikiendeshwa katika mahakama hiyo.

Alisomewa hukumu hiyo jana mbele ya Hakimu. Mkazi Ole Shadi Marwa katika kesi ya jinai namba 663/2023.

Hakimu Marwa alisema baada ya kusikiliza kesi hiyo, alikubaliana na mashahidi wa upande wa mashtaka kutokana na Ushahidi walioutoa bila kuacha chembe ya shaka.

"Kutokana na udanganyifu na uongo unaofanya hata mbele ya mahakama hii kusema uongo kuwa wewe ni wakili wa kujitegemea huku ukijua kuwa si wakili, nakuhukumu kwenda jela miaka miwili na kuchapwa viboko sita mara utakapoingia gerezani ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama wewe," alisema.

Awali, mwendesha mashtaka wa polisi, Sajenti Cosmas alidai kuwa katika kosa la kwanza Septemba 21, mwaka huu, Kasera alijifanya wakili jambo ambalo ni kosa chini ya kifungu cha Sheria namba 369 (1) cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Cosmas alidai kuwa shtaka jingine ni kutoa taarifa za uongo ambalo pia ni kosa chini ya kifungu cha 122cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Alidai kuwa wakati Hakimu Marwa akisikiliza kesi ya madai namba 189/2023 aliyokuwa akikabiliwa nayo Kasera kwa kudaiwa na Kikundi cha Luo Tarime kilichokuwa kikimdai na kufikishwa mahakamani hapo na kujitambulisha ni wakili msomi wakati si kweli.

Kabla ya hukumu hiyo, aliomba mahakama kumsamehe na kudai kuwa yeye si wakili bali anafanya kazi ya duka la kuuza vifaa vya shule na viandikia (stationery) mjini Tarime na Kikundi hicho cha Luo kilikuwa kinamdai wakati akiwa na msiba wa mzazi wake.

# Watendaji halmashauri wabainika kuhujumu miradi kuboresha shule

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imebaini baadhi ya watendaji wa halmashauri kuhujumu ujenzi wa miundombinu ya elimu inayotokana na mradi wa kuboresha shule za sekondari (SEQUIP) na mradi wa kuboresha shule za msingi (BOOST).

Miongoni mwa dosari zilizobainika katika miradi hiyo ni kukosekana uadilifu kwa baadhi yao kuingilia mchakato wa ununuzi. Hadi sasa shule 194 kati ya 302 kupitia mradi wa BOOST zimekamilika licha ya muda uliopangwa awali kuisha.

Akifunga kikao kazi cha Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya jana jijini hapa, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, alisema ofisi inajua kinachoendelea kwa baadhi ya halmashauri ambazo hazijakamilisha miradi hiyo.

"Mradi wa BOOST maelekezo tuliyokubaliana ilikuwa Juni 30 mwaka huu iwe imekamilika. Tulipiga kelele na mkafanya kazi, tukasogeza tena Julai. Leo hii ni miezi mitatu baada ya Juni 30 2023, lakini ni shule 194 tu zilizokamilika kati 302.

"Kuweni jasiri. Maofisa Elimu) simamieni sheria na taratibu zilizowekwa, hakuna fedha zinazoletwa kwenye halmashauri bila mwongozo. Mtu yeyote asikutoe kwenye reli, simamia maelekezo bila kuangalia mtu.

"Si kwamba hatujui kule chini mnavurugwa, mnatakiwa kusimama imara. Kuna halmashauri walipoona Sh. milioni 600 zimeingiwa wakapoka madaraka ya wakuu wa shule, wakaenda kufanya kosa kubwa la kiufundi, wakampanga mzabuni akaleta tofali mchanga na bei utata," alisema. Alifafanua kuwa ofisa elimu ambaye hakutaka kutaja jina lake, alikuwa jasiri -alikwenda kukagua matofali na kukuta ni mchanga. "Wakamjengea zengwe watu wa ununuzi na mhandisi wakampa kashkashi. Ofisa huyo akahamisha ofisi 'site' kwa kuanza kufyatua matofali, watu waliotegemea kupata donge mdomoni limeyeyuka hasira zimewakaba.

"Wakaenda kumshtaki kwa mkurugenzi na kumwita kuwa amevunja kanuni za ununuzi na kuharibu taratibu za ujenzi," alisema.

Alifafanua kuwa ofisa elimu huyo alimjibu mkurugenzi kuwa yeye ni bosi wake, anamheshimu, lakini hawezi kukubali matofali mchanga yajenge shule ya umma na yuko tayari kujiuzulu.

"Niwajulishe tu shule imejengwa, imeisha na mamilioni ya shilingi yamebaki. Huyu ofisa elimu ni mmoja wa majasiri ambao wamesimamia sheria na taratibu zinazowaongoza," alisifu. Dk. Msonde alisema kuwa ili miradi hiyo ikamilike, inahitaji juhudi, uzalendo na uadilifu na kama haikamiliki, hakuna hivyo vitu. "Heshimu viongozi waliopo juu yenu, lakini msiwaogope ili yale yanayoelekezwa na serikali yatekelezeke.

"Lengo la hii miradi ni ya Lipa Kulingana na Matokeo, tukija kukaguliwa na Benki ya Dunia (WB) wakakuta hivi, tumepigwa hatutapata fedha, mahitaji ya kujenga shule za msingi na sekondari ni makubwa mno," alisema.

Alikumbusha kuwa shule hizo zinapaswa ifikapo Desemba 31, 2023 ziwe zimesajiliwa na kuwataka waweke mafundi wa kutosha na kujenga usiku na mchana.

"Shule za SEQUIP na zile za sekondari kila mikoa zinatakiwa kukamilika kwa viwango vinavyotakiwa na kuwa zimesajiliwa si kubahatisha, shule hizi zitapangiwa wanafunzi. Ukifika muda ukasema haijakamilika utakuwa hutoshi," alionya.

Aliagiza maofisa hao kufanya tathmini ya miundombinu iliyokwama ikiwamo maboma yaliyojengwa na wananchi ili kupata gharama halisi.

"Fanyeni tathmini kupata gharama sahihi na ndogo ambazo serikali ikipata fedha itaweza kugharamia. Kwa mfano, miradi ya EP4R, na majengo yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu TAMISEMI, Vicent Kayombo, alisema katika kikao hicho wameangalia namna ya kuimarisha ubora wa elimu nchini na wamekubaliana ifikapo Desemba 31 mwaka huu kusiwe na wanafunzi wasiomudu stadi za kusoma.

HABARI KITAIFA

# Mirembe yaonya kukithiri unyanyapaa wagonjwa wa akili

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Lawala, amesema bado kuna kiwango kikubwa cha unyanyapaa katika jamii, hususan kwa wanaokumbwa na changamoto za afya ya akili, ikiwamo mazingira inakotolewa tiba ugonjwa huo.

Amesema dhana iliyoko katika jamii ni kuyanyooshea vidole maeneo yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya kutoa tiba, imesababisha Hospitali ya Mirembe kupewa majina tofauti yanayokuza unyanyapaa.

Mkurugenzi huyo ambaye pia ni Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili alibainisha hayo jana alipozungumza kuelekea Siku ya Afya ya Akili Duniani inayoadhimishwa Oktoba 10 kila mwaka.

"Ni dhana ya kihistoria na ya kidunia. Ni ugonjwa ambao unaleta madhara katika maisha ya mtu, hivyo anabadilika tofauti na alivyokuwa awali, unapunguza utu na thamani yake. Kwahiyo, eneo linalotibu linatafsiriwa kwamba ni ambalo linatibu watu wenye dosari.

"Ni dhana ambayo inabeba tafsiri kubwa kuwa wanaotibiwa pale (Mirembe) ni watu wenye kasoro. Ni unyanyapaa, kwamba ni eneo la hatari na wanaoingia pale wote maisha yao ndio basi tena, hawana thamani, ni dhana za kijamii," alisema Dk. Lawala.

Alisema sababu za matatizo ya afya ya akili zinaweza kujumuisha kunyanyaswa wakati wa utotoni, kuhisi upweke, kutelekezwa au kutengwa na jamii, kufiwa au kupoteza mtu wa karibu.

Alizitaja nyingine ni mazingira magumu kijamii, umaskini, madeni, kupitia shida ya aina yoyote kwa muda mrefu, kukabiliwa na ubaguzi, unyanyapaa pamoja na ubaguzi wa rangi.

"Pia kupitia matukio au hali ya kutisha, kuogofya na kusababisha kiwewe (trauma) nayo ni sababu ya magonjwa ya akili ambayo yapo ya aina zipatazo 200.

"Ni siku ya dunia ya kukumbushana kuhusu afya ya akili na kuelekezana na kuelekeza nguvu zetu katika kutafuta rasilimali ili jamii ipate elimu na ambao wanapitia tuone namna gani tunaweza kuwahudumia," alisema Dk. Lawala.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, takwimu za dunia zinaonesha kuwa katika mwaka 2021 watu walioathirika na aina mbalimbali za magonjwa ya akili duniani ni takribani milioni 979.

Tanzania inakadiriwa kuwa na takribani watu milioni saba wanaoishi na magonjwa ya akili.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2019, kila baada ya sekunde 40, kuna mtu anajiua kwa sababu mbalimbali na Afrika ina kiwango kikubwa zaidi cha watu wanaojiua duniani.

# ...Kasi wagonjwa wa akili yaongezeka

**Na Enock Charles**

WAGONJWA wenye matatizo ya afya ya akili wanaoripoti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, wameongezeka kutoka wastani wa watano hadi wanane hadi kufikia 30 hadi 45 kwa siku.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Zavery Benela, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana katika Wiki ya Afya ya Akili kilele chake ni Oktoba 10 mwaka huu ambayo ni Siku ya Afya ya Akili Duniani.

Alisema ongezeko la wagonjwa wa afya ya akili linatokana na visababishi mbalimbali vikiwamo vya kibaiolojia, kisaikolojia na kimazingira jambo ambalo alisema linahitaji kuongezwa wataalamu kulidhibiti.

"Kuanzia Juni, mwaka jana, tumeanza kupata ongezeko kubwa la wagonjwa wa afya ya akili ambalo linafikia wagonjwa 30 mpaka 45 kwa siku. Kabla tulikuwa tunapata wagonjwa watano mpaka wanane kwa siku jambo linaloonesha uhitaji wa kuwapo wataalamu wa magonjwa ya afya ya akili katika hospitali zetu," alisema Dk. Benela.

Alitoa wito kwa wataalamu wanaosomea fani za udaktari kusoma pia udaktari wa afya ya akili kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu hao kwa sasa kutokana na kasi ya ongezeko la wagonjwa ambalo haliendani na kasi ya ongezeko la wataalamu.

Kuhusu sababu ya kibaiolojia, alisema kisababishi ni kutokana na kurithi, magonjwa ya muda mrefu kama UKIMWI, kisukari na shinikizo la damu ambavyo husababisha mgandamizo wa mfumo wa ufahamu.

Alisema kiko pia kisababishi kinachotokana na kuvunjika kwa uhusiano, kushindwa kupata ajira kwa wakati na matatizo ya kifamilia ambayo huchangia mtu kufikiria kwa muda mrefu na kushindwa kuhimili changamoto zinazomkabili.

"Iko pia sababu ya kimazingira. Watanzania wengi tumekuwa tukiishi mazingira mabaya. Unakuta mtu anaishi katika chumba chake kama stoo, yaani sufuria humo humo, kitanda, kochi, redio hata usiku kinaweza kikaanguka kitu anapata mshtuko na kushindwa kupata usingizi. Hapo itamuathiri kisaikolojia. Wengine wanaishi na kulala barabarani," alisema.

Daktari huyo alisema umaskini wa kipato ni mojawapo ya sababu ya mtu kupatwa na ugonjwa wa afya ya akili pale anaposhindwa kukubaliana na hali halisi na kuchukua hatua zinazostahili kujikwamua.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## VACANCY ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the position mentioned below:

**1. POSITION: RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT I (1 POST)**

**1.1 QUALIFICATIONS**

- Must be a holder of Diploma in one of the following fields: Records Management, Records and Archives Management, Corporate Information Management, or equivalent qualification from recognized institutions.
- Must have working experience of at least four (4) years in related field.

**1.2 RESPONSIBILITIES:**

i. Ensure that a file register is in place.
ii. Receive incoming mail, stamp and record them in relevant register.
iii. Send mail preview box to preview officers and record daily movement of files
iv. Ensure letters have all attached documents referred to; and letters are signed by relevant desk officers after attending to them
v. Ensure that envelopes are affixed with proper stamps and are addressed correctly
vi. Circulate flimsy files to the authorized officers.
vii. Develop individual objectives/targets and performance standards as part of the individual performance agreement in consultation with the immediate superior.
viii. Perform any other official duties as provided by the supervisor.

**2. TERMS AND CONDITIONS:**

Ten (10) years contract with attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**3. MODE OF APPLICATION:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the applications attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School and birth certificate), and other relevant certificates and licenses. (Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities i.e Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council- NECTA))
iii. Two recent passport size photographs;
iv. Names and addresses of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.

Note: Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences.
Previous applicants may re-apply.

**4. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement: -

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhalilishaji huu dhidi ya watoto uchukuliwe hatua

**KATIKA** mikusanyiko mbalimbali ya kijamii hasa sherehe za harusi na zile za kuwaaga mabinti kwenda kuanza maisha ya ndoa, kumekuwa na burudani mbalimbali zikiwamo muziki na ngoma. Baadhi ya burudani hizo, ambazo nyingi hufanyika wakati wa usiku, zimekuwa zikiwahusisha pia watoto kucheza muziki na shoo mbalimbali.

Watoto wanaoshiriki katika sherehe hizo, wanapocheza muziki au shoo, baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwarekodi na kuwaweka kwenye mitandao ya kijamii na umma wa watu dunia nzima hushuhudia. Hatua hiyo imekuwa ikisababisha watu mbalimbali kutoa maoni yao yakiwamo yale yanayodhalilisha utu wa mtu kutokana na mazingira ambayo baadhi ya watoto huwekwa ikiwamo kuvaa mavazi yasiyo na staha.

Kuwapo kwa hali hiyo kumesababisha jamii na viongozi waandamizi serikalini kukemea na wakati mwingine kutoa matamko kwamba ni marufuku kuwatumia watoto katika matukio kama hayo. Jana kwa mfano, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alikemea vitendo vya baadhi ya wazazi kuwarekodi watoto wakiwa wanaimba na kucheza kuweka picha na video zao kwenye mitandao ya kijamii. Kunenge alitoa kauli hiyo alipokuwa akizundua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto kwa Mkoa wa Pwani.

Bila kuuma maneno, Kunenge alisema vitendo hivyo havileti mafundisho mazuri katika jamii na kuwataka wazazi kuacha tabia hiyo mara moja na badala yake kusimamia malezi kwa watoto. Aliweka bayana kwamba kitendo cha kuwarekodi watoto na kusambaza video kina athari kubwa kwa mtoto kwa siku za baadaye, hasa atakapokuwa mkubwa kutokana na ukweli kwamba zinaweza kutumika kama rejea katika baadhi ya mambo.

Hii si mara ya kwanza kwa viongozi wa serikali kukemea vitendo hivyo. Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima aliwahi kuweka bayana kwamba watoto kutoruhusiwa kucheza shoo' kwenye sherehe hasa nyakati za usiku.

Gwajima alitoa kauli hiyo miaka michache iliyopita baada ya kusambaa kwa video mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, zikionyesha watoto wakitoa burudani kwenye sherehe wakati wa usiku na katika miondoko isiyofaa kwa umri wao.

Pamoja na kupiga marufuku hiyo, alisisitiza kuwa mambo hayo ni kinyume cha Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 iliyorekebishwa mwaka 2019 ambayo inazuia kumtumia mtoto kwenye maonyesho ya harusi, mitindo ya nguo au maonyesho mengine kama hayo wakati wa usiku. Licha ya kubainisha kuwa sheria hiyo inakataza watoto kushiriki katika masuala hayo, alisema watakaobainika kufanya hivyo, adhabu yake ni faini ya Sh. laki tano au kifungo cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja.

Kwa ujumla, suala hili limesemwa na kukemewa na viongozi mara kwa mara na sasa kinachotakiwa ni utekelezaji ili wazazi au watu watakaobainika kuhusika na vitendo hivyo, wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria. Haiwezekani kuona kwamba jambo limekuwa likikemewa mara kwa mara lakini wazazi bado wanaendelea kuwatumia watoto katika maeneo yasiyofaa huku viongozi wakizungumza tu badala ya kuchukua hatua.

Ni dhahiri kwamba serikali ina macho kila sehemu na mikono mirefu kuiwezesha kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka sheria zilizowekwa zikiwamo za kuwalinda watoto dhidi ya madhara yanayoweza kuwakumba, hivyo ni wakati sasa wa kuchukua hatua kuliko kuendela kuzungumza.

Wahenga wanasema mzaha mzaha hutumbua usaha, hivyo jambo la msingi ni kwamba vitendo kama hivyo visiendelee kusikika au kukemewa na viongozi badala yake wanaoendelea kuvikumbatia wachukuliwe hatua ili iwe fundisho kwa wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mama lishe mitaani kwetu, nanyi maofisa afya, kuna shida ya usafi

Na Mary Seme

**UKIPITA** baadhi ya mitaa ya Dar es Salaam hasa ya kule 'uswahilini' utawaona baadhi ya kinamama maarufu 'mama ntilie', ingawa huo ni msamiati marufuku, ruksa iko katika mama lishe'

Hapo utawaona wanajipatia riziki kwa shughuli ya upishi wa chakula na kwa wasio na fedha ya kuikodisha fremu za za biashara, wanajenga vibanda vya mbao na kununua miamvuli ya jua tu tayari inatosha kufanyia huduma zao.

Kikawaida biashara ya chakula inahitaji usafi wa kiwango cha juu kuanzia mavazi, mazingira yanayozunguka na vyombo vinavyotumika kupika na kupakuliwa chakula, lakini imekuwa tofauti kwa baadhi ya mama lishe.

Siajabu kukuta mazingira pamesheheni uchafu katika biashara na kwa bahati mbaya, wahusika wa kuwasimamia ni kama wamelala au wamewapuuzia au sijui nisemeje?

Ninavyofahamu kwa biashara za aina hiyo, ni muhimu kwa bwana afya au bibi afya kupita kukagua mazingira ya biashara kila mara, ili kuhakikisha zinafanyika katika mazingira safi na salama kwa walaji .

Vinginevyo wataendelea tu kufanya kazi zao kwa mazoea, kwa kuwa baadhi yao hawana uelewa kuhusu masuala ya usafi anachojua yeye, ni kupata fedha tu.

Unaweza kupita mahali usiamini kuwa watu wanajipatia chakula katika mazingira hayo. Utakuta mabaki ya chakula yakiwa yamemwagwa hovyo kuzunguka jirani na vibanda vya kuuzia chakula , vyombo vichafu vimerundikwa nje vikilambwa na mbwa na wenyewe wakaona ni sawa tu.

Mara nyingi watu wanaohusika na kukagua usafi wa kina- mama lishe utawaona pakitokea mlipuko wa maradhi kama kipindupindu au ugonjwa mwingine.

Yapo magonjwa mengine ambayo pengine hayaonekani sana na hayapewi kipaumbele, lakini yana athari za afya, baadhi ya Watanzania wenzetu wakiangukia foleni katika zahanati na vituo vya afya, kwa sababu tu ya kutozingatiwa usafi huo.

Mtu anaweza asipate kipindupindu, lakini anaugua tumbo kila mara, hivyo anabaki muhanga wa kutumia dawa kila wakati.

Dawa kama vile 'Flagyl' ni maarufu miongoni mwa Watanzania pengine ni kutokana na watu kuzoea kuugua tumbo, kutokana na kula uchafu jambo linaloweza kudhibitiwa kwa kuzingatia tu usafi wa mazingira na vyombo vya kulia chakula.

'Kinga ni bora kuliko tiba'. Kama inawezekana kufanya usafi na kuepuka magonjwa ni kwanini ndugu zetu hawa wanashindwa kuzingatia usafi ?.Ni wakati sasa wahusika ikiwemo mabwana afya na mabibi afya kuchukua hatua ili kuthibiti tatizo hili sugu katika sehumu mbalimbali za kuuza chakula katika jiji la Dar es Salaam.

Mamlaka zinazohusika na kutoa vibali kwa biashara ya Mama/Baba Ntilie ni vyema kuwasisitiza kuhusu suala la usafi , wajue kwamba usafi ni moja ya vipaumbele muhimu katika biashara hizo. Miaka kadhaa iliyopita nikiwa naishi mkoani Tabora nilikuwa nikishuhudia mabwana afya wakifanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika sehemu zinakofanyika biashara za chakula.

Mabwana afya walikuwa wakali kweli kweli wakikuta mathalan hakuna maji ya moto ya kunawia wateja, vyombo havioshwi inavyopaswa , mama au baba ntilie haujavaa 'apron' basi utakiona cha mtema kuni walikuwa hawasiti kufunga biashara muda huo huo kama wakikuta vigezo havijazingatiwa na mtoa huduma ya chakula, hiyo ilikuwa ikisaidia sana kuweka mambo sawa tofauti na siku hizi ambapo ni nadra kuwashuhudia wakipita mtaani kufanya ukaguzi wa kiwango hicho.

Ni vyema kuzingatia kwamba katika masuala ya afya kama mmoja hayupo salama basi uwezekano ni mkubwa kwa wote wanaomzunguka kutokuwa salama pia na ndiyo maana pakitokea mlipuko panawekwa tahadhari maalumu katika eneo husika ili ugonjwa usienee , afya ya mtu mmoja inaweza kuwagharimu mamilioni ya watu.

# RC akemea wazazi kuwarekodi watoto, kuwaweka mitandaoni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amekemea vitendo vya baadhi ya wazazi kuwarekodi watoto wakiimba na kucheza na kuweka picha na video zao kwenye mitandao ya kijamii.

Amesema vitendo hivyo havileti mafundisho mazuri katika jamii na kuwataka wazazi kuacha tabia hiyo mara moja na kusimamia malezi kwa watoto wao badala ya kuacha jukumu hilo kwa wasichana wasaidizi wa ndani.

Kunenge aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akizindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto kwa Mkoa wa Pwani.

Alisema kitendo cha kuwarekodi watoto na kusambaza video kimekuwa kikimuumiza kama mzazi kwa kuwa baadhi ya nyimbo wanazoimba watoto hao na umri wao ni tofauti na kwa kuwa teknolojia inaishi, miaka ya baadaye inaweza kusababisha athari kwa watoto hao.

Kunenge alisema ni lazima wazazi na walezi wawe karibu na watoto kufuatilia maendeleo sambamba na kuwakagua mara kwa mara kazi zao za darasani badala ya kuacha wajibu huo kufanywa na wasaidizi wa kazi.

"Tunakimbizana sana na mambo ya hela kuliko watoto. Mtoto sasa yuko karibu zaidi na dada wa kazi kuliko wazazi wake. Dunia inabadilika siku hizi wazazi wengi hawapendi kuwajibika, lazima tukumbuke suala la malezi ya watoto pia ni ibada," alisema.

Katika hatua nyingine Kunenge ameziagiza halmashauri za mkoa wa Pwani kutenga bajeti kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa programu hiyo pamoja na kutoa elimu kwa jamii ya kuwaweka watoto salama.

Janet Christian, kutoka Taasisi ya Anjita ambayo inashirikiana na Ofisi ya Mkoa wa Pwani katika utekelezaji wa programu hiyo ya malezi, alisema wamejikita zaidi kuwajengea uwezo wananchi kuhusiana na malezi.

Alisema taasisi hiyo inajishughulisha na kuhamasisha uwapo wa vifaa vya michezo kwenye vituo vya malezi na kwamba baada ya uzinduzi huo, wanatarajia kufika hadi ngazi ya mtaa kuimarisha huduma bora za malezi na makuzi. "Jamii bado haina uelewa kuhusiana na malezi katika utekelezaji wa programu hii, tutahakikisha kunakuwa na ushirikiano kati ya wadau wote wanaohusika ili wafanye kazi kwa pamoja," alisema.

Isack Idama kutoka Shirika la Children In Crossfire, alisema mtandao wa malezi kwa kushirikiana na wadau wengine, walikaa pamoja wakaona ni vyema kuja na programu jumuishi ambayo itawaleta wadau wote wanaofanya kazi na mambo ya watoto zikiwamo wizara za kisekta, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, na Wizara ya Fedha.

Alibainisha kwamba wizara zingine za kisekta zimeungana ili kutengeneza hiyo kwa kutambua mtoto mwenye miaka sifuri hadi minane anapata huduma stahiki kama vile afya, lishe bora, ulinzi na usalama, ujifunzaji wa awali pamoja na mwitikio chanya. Alisema wanaamini kwamba maeneo hayo matano endapo yatatekelezwa kwa ukamilifu, mtoto atakuwa na tija baadaye.

Helen Mapambano, mwanafunzi wa darasa la sita Shule ya Msingi Kambarage, alisema wazazi wanatakiwa kujenga tabia ya kutowahusisha watoto kushiriki shughuli mbalimbali zinazoambatana na muziki.

Alisema kitendo cha watoto kushiriki kwenye shughuli kinawafanya kuiga mambo mengi ambayo hayaendani na umri wao na hivyo kukua katika maadili hayo wakiiga kila wanachokiona.

# Mawakala waomba ziada viwango utoaji fedha

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAWAKALA wa fedha wa CRDB Tawi la Kahama mkoani Shinyanga, wameiangukia benki hiyo kwa kuiomba kuongezewa viwango vya utoaji wa fedha kwa wateja wao kutoka Sh. milioni 10 hadi milioni 30 ili kupunguza msongamano wa wateja.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Huduma kwa wateja iliyofanyika ndani ya benki hiyo kwa kujumuisha wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo na wateja wa kawaida.

Mmoja wa mawakala hao, Mohamed Chalila, alisema wamekuwa wakipata wateja wengi wenye kuhitaji viwango vikubwa vya fedha lakini kutokana na kikomo cha kiwango wanachotoa cha Sh. milioni 10, inawalazimu kuwataka kwenda benki. Kutokana na hali hiyo, aliuomba uongozi wa benki hiyo kurekebisha viwango ili wawe wanatoa hadi Sh. milioni 30.

"Mteja anapofika kuchukua fedha kiwango kikubwa ambacho hatuwezi kukitoa, inasababisha sisi kukosa wateja kwa sababu atakimbilia benki. Tunaomba hili mtusaidie ili tuwe na uwezo wa kutoa zaidi hadi Sh. milioni 30 ikiwezekana," alisema.

Padri wa Kanisa la Katoliki Jimbo la Kahama, Wilbroad Kibozi, alipongeza huduma nzuri kwa wateja na kusababisha kuwa na wateja wengi. Hata hivyo, alishauri benki kusikiliza malalamiko ya wateja na kuyatatua kwa wakati ikiwamo kuongeza viwango vya utoaji fedha kwa mawakala.

Meneje wa CRBD Tawi la Kahama, Erick Chambanenge, alisema waliweka kikomo cha utoaji wa fedha kwa mawakala cha Sh. milioni 10 kulingana na hali ya usalama wa maeneo yao kwa sababu hawana polisi anayewalinda wala kampuni za ulinzi kama ilivyo katika taasisi za kifedha.

Alisema wakala atakayekidhi hali ya usalama wa fedha eneo lake la biashara, anaweza kufika benki la kuomba kuongezewa viwango vya fedha anavyovihitaji na benki itamhudumia.

ZRA
ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY
MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

## TAARIFA KWA UMMA

### KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO

**Zanzibar, 30 Septemba, 2023.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), inaufahamisha umma kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78) kuhusu viwango maalum vya kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024 kwa mujibu wa kifungu cha 7A (1) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam.14 ya Mwaka 2008.

Tangazo la Kisheria la kutoza kodi ya majengo kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, **LIMESAMEHE KUTOZWA KODI YA MAJENGO kwa MAJENGO YA MAKAAZI yasiyo ya Ghorofa.**

Majengo yafuatayo yatatakiwa kulipa kiasi maalum cha kodi kama ilivyoainishwa katika Jadweli hapa chini:

| SN | AINA YA JENGO | KIASI CHA KODI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Majengo ya ghorofa ya makaazi au kondominiam | Tzs. 10,000/= kwa kila ghorofa au Jengo (Unit) |
| 2. | Majengo ya biashara yenye ghorofa | Tzs. 50,000/= kwa ghorofa |
| 3. | Majengo mengineyo ya biashara | Tzs. 50,000/= |
| 4. | Majengo ya hoteli:<br>(a) Hoteli ya nyota tano<br>(b) Hoteli ya nyota nne<br>(c) Hoteli ya nyota tatu<br>(d) Hoteli ya nyota mbili<br>(e)Hoteli ya nyota moja<br>(f) Hoteli nyenginezo | <br>Tzs. 500,000/=<br>Tzs. 400,000/=<br>Tzs. 300,000/=<br>Tzs. 200,000/=<br>Tzs. 100,000/=<br>Tzs. 50,000/= |

**2.0 MUDA WA KISHERIA WA KULIPIA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya Mwaka 2008, kiasi chote cha kodi ya majengo kwa mwaka kinapaswa kulipwa kabla au siku ya tarehe **30,Septemba** ya kila mwaka, na si zaidi ya tarehe **30, Juni** ya mwaka unaofuata.

**3.0 KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha Sheria kilichotajwa hapo juu, kodi ya majengo inalipwa kabla au siku ya tarehe 30, Septemba, 2023. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba, viwango vya kodi ya majengo vimeanzishwa hivi karibuni chini ya alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), hivyo basi hii ni sababu ya msingi na yenye kutosheleza kuongeza muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024.

Kwa muktadha huo, na kwa mujibu wa kifungu cha 10 (2) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008, tarehe ya mwisho ya kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024, imeongezwa kutoka siku ya tarehe ya 30 Septemba, 2023 hadi siku ya tarehe 30 ya Novemba, 2023.

**4.0 MADHARA YA KUTOLIPA KODI YA MAJENGO KWA WAKATI:**

Mmiliki yeyote wa jengo lililo miongoni mwa majengo yaliyoorodheshwa katika Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), anapaswa kulipa kodi ya majengo kabla au siku ya tarehe 30, Novemba,2023, ili kuepuka adhabu kama ilivyotolewa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi, Na. 7 ya 2009.

**5.0 HITIMISHO:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar inawataka wamiliki wa majengo husika kutumia vizuri nyongeza ya muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo katika kutimiza wajibu wao.

Wakati huo huo, ZRA, itaanza kampeni ya uhamasishaji na utaratibu wa ulipaji kodi hii kwa wamiliki wote wa majengo husika ili kuongeza uwajibikaji wa hiari kabla ya tarehe ya mwisho ya kulipa kodi. ZRA inawahakikishia wamiliki wote wa majengo kuendelea kuchukua hatua za kisheria zinazofaa katika kurahisisha ulipaji kodi ya majengo kwa hiari.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

Yusuph Juma Mwenda
**Kamishna Mkuu**

SLP 2072,
SLP 163 (P)
255-24-245255 (
255-24-2233041
www.zanrevenue.org
1 Barabara ya Fumba, 7112 5 Mjini Magharibi, Zanzibar
262 Barabara ya Chake-Wete, 74206 Wara, Kusini Pemba, Zanzibar (P)
zra@zanrevenue.org

# Waziri Silaa aagiza mpango uendelezaji viwanda

**Na Munir Shemweta,**
KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameagiza kuwapo mpango wa uendelezaji eneo la viwanda lililoko Kibaha vijijini, mkoani Pwani.

Silaa ametoa agizo hilo juzi Mlandizi wakati alipokagua miundombinu ya Kongani ya Viwanda Kibaha ambayo mmoja wa wawekezaji ni kampuni ya ya KAMAKA Limited.

"Mhakikishe sasa kwa kuwa Pwani inakua na ndiyo eneo la viwanda katika taifa letu, tuhakikishe maeneo yetu yote ndani ya kongani hii ya viwanda kunaandaliwa mpango mkubwa wa uendelezaji," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa, mji unapokuwa wa viwanda, lazima uwe unajitosheleza kwenye maeneo yote na kubainisha kuwa wakati eneo la kongani ya viwanda likifanyiwa kazi, halmashauri ziendelee kushughulikia kijamii na kuhamasisha watu huku akisisitiza kuwa si kila mwekezaji anayekuja anataka kuwekeza kwenye eneo la viwanda.

"Kumbe kwa uwekezaji huu mwekezaji anaweza kujenga nyumba za makazi, zikapata wateja kuliko hata nyumba zilizoko Dar es Salaam kwa sababu hapa viko takriban viwanda 202 vina wafanyakazi watakaohitaji makazi na hao wanaweza kupata nyumba zikawasaidia kupata maeneo ya kuishi," alisema.

Meneja Mradi wa Kongani ya Viwanda Kibaha, Nelson Mollel, alisema lengo la mradi huo ni kuitikia wito wa serikali kujenga viwanda, kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya watu kupitia uwekezaji.

Aliweka wazi kuwa teknolojia mpya pamoja na kuongeza fursa za kiuchumi katika kuongeza ajira na kulinda hifadhi ya mazingira na kujenga viwanda vingi eneo moja badala ya kuwa na viwanda vingi vilivyotawanyika maeneo mbalimbali, ni sehemu ya malengo ya mradi.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Simon Nikson, alisema wilaya imetenga maeneo kwa ajili ya viwanda kwa lengo la kutaka uwekezaji sambamba na viwanda huku akibainisha kuwa watu wakipita eneo hilo wanajua ni kiwanda wakati ni miundombinu iliyoandaliwa kwa ajili ya Kongani ya uwekezaji viwanda.

Kwa mujibu wa Nikson, eneo hilo linatarajiwa kuwa na takriban viwanda 200 na huduma zote za msingi za viwanda zinapatikana na kubainisha kuwa taasisi kama Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zitatoa huduma kwenye jengo moja.



Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Simon Nikson (kushoto), akimuelekeza jambo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (katikati), alipotembelea Kongani ya Viwanda Kibaha, mkoani Pwani juzi. **PICHA: WANMM**

# Mwanafunzi kortini madai kujeruhi mwalimu

**Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MWANAFUNZI Alex Lameck wa Shule ya Sekondari Tamabu, amepandishwa kizimbani kwa tuhuma za kumjeruhi kwa kumkata panga kichwani mwalimu wake, Stamford Magaya.

Lamech anadaiwa kufanya kitendo hicho wakati mwalimu akiwa ofisini baada ya kumrejesha nyumbani kwenda kunyoa ndevu na kuvaa viatu.

Mwanafunzi huyo alifikishwa kizimbani jana katika Mahakama ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza na kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Evod Kisoka. Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Morice Mtoi, alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Septemba 25, 2023 katika Shule ya Sekondari ya Tamabu kwa kumjeruhi mwalimu huyo na kumsababishia jeraha.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo huku mwendesha mashtaka akidai kuwa ushahidi wa kesi hiyo uko tayari na upande wa mashtaka uko tayari kuanza kuwasilisha.

Hakimu Kisoka aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 11, mwaka huu, kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali na kupokea ushahidi kuhusu shauri hilo.

Mshtakiwa Lameck yuko nje kwa dhamana na aliruhusiwa kuendelea na masomo wakati kesi hiyo ikiendelea.

# TAKUKURU, DECEA zaagizwa kutoa elimu kwa wananchi vijijini

**Na Peter Mkwavila** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na na Dawa za Kulevya (DCEA) zimetakiwa kutoa elimu kwa jamii na klabu za kupinga vitendo hivyo katika shule na vyuo ili kufikia malengo ya kukomesha vitendo hivyo nchini.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa (TAKUKURU) Kamishna Salum Hamduni, alipokuwa akizindua kampeni ya tokomeza rushwa na dawa za kulevya shuleni na vyuoni kwa watumishi wa taasisi hizo uliofanyika jijini hapa.

Mkurugenzi huyo aliwataka watumishi hao waliopatiwa mafunzo hayo, kuishusha elimu hiyo hadi ngazi ya chini kwa klabu za wapinga rushwa vyuoni, shuleni na kwenye jamii ili kukabiliana na vitendo hivyo vya matumizi ya dawa za kulevya na rushwa.

Alisema, elimu hiyo anaamini itawakomboa wale wanaojihusisha na vitendo hivyo ikizingatiwa kuwa imekuwa ikidhohofisha na kuleta madhara kiuchumi kijamii kisiasa pia na nguvu kazi ya taifa.

Mafunzo hayo, alisema yakawe mkombozi katika kuwaokoa wale wanaojihusisha na vitendo ambavyo vimekuwa vikisababisha kupoteza mapato, vifo na gharama kwa serikali katika kuwahudumia.

"Watumishi ambao mmepata mafunzo haya kwa taasisi hizi mbili mkaweze pia kubadilishana taarifa zitakazowawezesha kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya na mapambano dhidi ya rushwa.

"Rushwa imekuwa kichocheo kikubwa cha kukua kwa dawa za kulevya hapa nchini na duniani kwa ujumla, hivyo ni mategemeo yetu mtaenda kuweka wigo mkubwa na nguvu ya pamoja katika kukabiliana na kudhibiti mapambano tatizo la biashara ya dawa hizo za kulevya," alisisitiza.

Awali, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za kulevya, Aretas Lyimo, alisema lengo la kuzikutanisha pande zote mbili ni kuwajengea uwelewa wa kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya na rushwa, vitendo ambavyo vimekuwa vikiathiri ukuaji wa uchumi.

Pia, alisema hali hiyo itawawezesha kupitia nafasi zao kuwapunguza watumiaji wa dawa za kulevya na vitendo vya rushwa na hatimaye kupatikana nguvu kazi zitakazokuwa na uzalendo na kuimarisha uchumi ya nchi.






Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia), akifurahia jambo na Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja (kushoto), baada ya kukagua miradi ya maendeleo iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru juzi, ambao kilele chake kitakuwa Oktoba 14 mwaka huu, mjini Babati. **PICHA: GIFT THADEY**

# TAWA yatwaa mashamba matatu ya mwekezaji Monduli

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA), imeyatwaa rasmi mashamba matatu makubwa maarufu kama mashamba ya 'Stain' yaliyokuwa yakimilikiwa na mwekezaji raia ya kigeni katika Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha.

Mashamba hayo, ambayo ni amani lenye ekari 9,007, lente ekari 3,344 na loldebes ekari 2,812, sasa yatatumika kama eneo maalum la kuendeleza shughuli za uhifadhi na utalii.

Jana, Mkurugenzi wa Ubinafsishaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mohamed Nyasama, alisema Februari 27 mwaka huu, serikali ilitoa maelekezo mashamba hayo yakabidhiwe kwa TAWA, kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uhifadhi na utalii.

Serikali iliyataifisha mashamba hayo mwaka 1981 na hisa zake zote kuhamishiwa hazina iliyoko chini ya Wizara ya Fedha.

"Maelekezo ya mamlaka yapo very clear (yanaeleweka) kuwa mashamba hayo ya STAIN yanakabidhiwa kwa TAWA, kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa utalii na siyo vingine," alisema.

Aidha, alisema eneo hilo limekabidhiwa kwa TAWA, kutokana na mashamba hayo kutolimwa kwa muda mrefu, hali ya ikolojia yake ilibadilika kukosa sifa ya kuwa mashamba ya kilimo, na kuwa msitu wenye aina mbalimbali za wanyama pori.

"Kutokana na hali ya utulivu wa mashamba hayo yaliyopo kwenye ushoroba unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Manyara, Ranchi, Ziwa Manyara na Msitu wa Hifadhi ya Essimingor hupenda kutumiwa na wanyama kama eneo la mazalia,"alisema

Baada ya kukabidhiwa mashamba hayo, Kamishna wa Uhifadhi kutoka TAWA, Mabula Nyanda, aliishukuru serikali kwa kukubali TAWA, kukabidhiwa eneo hilo kwa ajili ya kulilinda, kuhifadhi na kuendeleza shughuli za utalii.

"Imani hiyo kubwa kutoka kwa serikali kwa TAWA, imetupa matumaini makubwa na sisi tuna deni la kulipa. Nimwakikishie kuwa tunasimamia eneo hili kwa ubunifu mkubwa kuhakikisha kuwa tunalihifadhi na kuongeza mapato ya nchi pamoja na wananchi wanaozunguka eneo hilo," alisema

Kwa mujibu wa Nyanda, kutokana na shughuli mbalimbali za utalii zitakazofanyika katika mashamba hayo kuanzia sasa, yatajulikana kwa jina la "Makuyuni Wildlife Park na itakuwa ni bustani ya wanyama ya kipekee duniani.

Alisema wamejipanga kikamilifu kuhakikisha wanaiendeleza kwa ubunifu wa kipekee.

Nyanda, alitaja shughuli hizo kuwa ni pamoja na utalii wa 'Night Game Drive' utalii wa ndege wa kipekee waliopo katika eneo hilo, utalii wa kupanda balloon, utalii wa kutembea kwa kupanda milima, bush dinner, walking safaris, na utalii wa kitamaduni.

Alisema wameligawa eneo hilo katika sehemu kuu mbili, ambazo ni eneo la matumizi maalum na eneo la matumizi ya jumla kwa kuzingatia rasilimali zilizopo na hii imevutia wawekezaji wengi, kuomba kuwekeza katika eneo hilo na taratibu zinaendelea.

Alitaja wanyama wanaoonekana eneo hilo, kuwa ni pamoja na tembo, simba, chui, twiga, punda milia, mbwa mwitu pamoja na aina mbalimbali za swala.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Joshua Nassari, aliishukuru serikali kwa kutoa eneo hilo kwa TAWA, ambalo limekuwa na mgogoro wa muda mrefu.

Alisema ana imani kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, itapata mgawo wa mapato kutoka TAWA, yanayotokana na shughuli zitakazofanyika katika eneo hilo.

# Serikali yatenga bil. 5/- kuwawezesha vijana kiuchumi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiinua kiuchumi.

Aliyasema hayo katika Mji wa Babati, mkoani Manyara baada ya kukagua uwanja mpya utakaotumika kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru, Oktoba 14 mwaka huu.

Alisema serikali imeshawawezesha Sh. bilioni moja kutokana na marejesho Ofisi ya Waziri Mkuu imeshatoa Sh. bilioni 2.8 kwa vijana.

Aidha, alisema serikali inatakiwa kutoa Sh.bilioni tisa ili kuwajengea ujuzi vijana ambapo inaangalia sekta za utalii, mapishi na ujasiriamali.

"Tumekuwa tukitoa fedha kwa mafunzo ya unajenzi kwa vijana na ni kwa waliomaliza vyuo vikuu na vyuo vya kati,"alisema Prof. Ndalichako.

Vilevile, alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 watawaingiza vijana 1,500 ambapo bajeti ya mwaka huu ni Sh. bil. 9 ila wameshapewa Sh. bilioni tano.

Aliongeza kuwa wakuu wa mikoa yote kuangalia namna ya vijana kufika Manyara kwenye wiki ya vijana ili waweze kupata fursa.

Awali, Katibu Mku, Ofisi ya Waziri Mkuu, Cyprian Luhemej, aliwaomba vijana wote kufika Manyara ili kwenye wiki ya vijana wajadiliane namna ya kupata ajira ndani na nje ya nchi.

Luhemeja alisema wakifika wataweza kupunguza kulalamika maana wataziona fursa za ajira.

# BRELA, SIDO waagizwa kufungua ofisi katika halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,**
PANGANI

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exhaud Kigahe ameziagiza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO), kufungua ofisi katika ngazi za halmashauri ili kuwahudumia wafanyabiashara wengi zaidi.

Alitoa agizo hilo jana, wakati akifunga Kongamano la Biashara na Uwekezaji katika Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, lililowakutanisha wafanyabishara mbalimbali mkoani Tanga.

Alisema kwenye ngazi za halmashauri kuna wafanyabiashara wengi ambao wangependa kurasimisha biashara zao lakini wanashindwa kutokana na kukosekana kwa ofisi za taasisi husika.

"Ni muhimu SIDO, BRELA mkaweka watu wenu hadi ngazi za halmashauri ili kuwezesha wale wajasiriamali na wafanyabiashara wanaotaka kurasimisha biashara zao wafanye hivyo kwa urahisi zaidi," alisema Kigahe.

Aidha, Kigahe alisema serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili sekta binafsi zifanye vizuri katika maendeleo ya biashara na uchumi.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara, wadau wa maendeleo na wajasiriamali kuchangamkia fursa za utalii, kilimo, ufugaji na uchumi wa buluu zinazopatikana katika Wilaya ya Pangani.

Vilevile, alisema ni wakati sasa thamani ya malighafi nchini iongezeke iwe maradufu na nchi iweze kuzalisha bidhaa zilizokamilika ili ziweze kuingia katika soko huru la biashara Afrika na masoko mengine ndani na nje ya Afrika

Kadhalika, alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainab Issah, kwa maandalizi ya kongamano hilo, akisema ni Mkuu wa Wilaya wa kwanza nchini kuanda 'Pangani Royal Tour' itakayofungua milango katika vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Saadani, zao la mwani, uchumi wa buluu, kilimo na ufugaji.

Baada ya ufunguzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainab Issah, aliishukuru serikali kwa kuifungulia maendeleo Pangani, hasa katika ujenzi wa Barabara Tanga- Pangani-Saadani-Bagamoyo, Daraja la Mto Pangani pamoja na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema ujenzi wa barabara hizo ni nguzo muhimu kwa ustawi wa mkoa huo, kwa kuwa zitahamasisha uwekezaji na mwingiliano wa kibiashara ndani na nje ya nchi.



# Ofisa biashara anyimwa dhamana kesi ya ubadhirifu milioni 409/-

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

WAKATI washtakiwa wawili maofisa wa Halmashauri ya Bukoba wakipata dhamana katika kesi ya ubadhilifu wa Sh. milioni 409 inayowakabili maofisa watatu wa halmashauri hiyo, Ofisa Biashara wa Halmashauri hiyo, Richard Kubona amekosa dhamana hiyo kwa kutokukidhi vigezo.

Kwa mujibu wa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Bukoba, Daniel Yona kesi hiyo iliposomwa kwa mara ya pili mahakamani hapo alieleza kuwa ofisa biashara huyo hawezi kupata dhamana kutokana na makossa yake kuwa ya uhujumu uchumi. Alisema kuwa katika kesi hiyo Kubona anakabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi na kutakatisha fedha ambayo haina dhamana kisheria, huku washtakiwa wengine ambao ni Adelina Kasigwa na Mussa Kalumba wakipata dhamana kutokana na makossa yao kuwa tofauti.

"Watuhumiwa hawa wengine dhamana zao ziko wazi kwani wanakabiliwa na kesi ambayo aiusiani na uhujumu uchumi na kutakatisha fedha, bali wao wanakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya mdaraka na kufoji nyaraka za serikali na kumdanganya mwajili kinyume cha sheria,"alisema Hakimu Yona.

Aidha, alisema kuwa dhamana hiyo ilitolewa kufuatia vigezo na mashariti vilivyotolewa na Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Bukoba na waliopata dhamana wamekidhi vigezo hivyo.

Maofisa hao kutoka kitengo cha biashara katika Halmashauri ya Bukoba walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza mwishoni mwa Septemba mwaka huu wakikabiliwa na makossa mbalimbali yakiwemo ya uhujumu uchumi.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kutoa leseni feki za biashara za Sh.milion 409 ambapo kesi hiyo iliishia kutajwa kutokana na Mahakama hiyo kutokua na mamlaka kisheria ya kusikiliza.

Hivyo, ofisa huyo alirudishwa rumande kusubiri kesi hiyo itakapo tajwa kwa ajili ya kusikilizwa tena.

# DC apokea malalamiko 200, mengi kuhusu migogoro ya ardhi

**Na Vitus Audax,** UKEREWE

KERO zaidi ya 200 zimepokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko katika siku mbili za operesheni tatua kero, huku baadhi ya kero hizo zikitatuliwa moja kwa moja na nyingine zitatuliwa wakati mkuu huyo wa wilaya atakapofika katika maeneo husika.

Kero hizo zilianza kusikilizwa juzi na jana katika viwanja vya Gertrude Mongella wilayani hapa, zikichukua siku mbili kutokana na wingi wake, asilimia 90 ya kero hizo zikiwa ni za migogoro ya ardhi baina ya wananchi kwa wananchi na wananchi kwa halmashauri.

Miongoni mwa migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro wa Tagile Mkama na wenzake 14 walioeleza kuidai halmashauri hiyo fidia ya ardhi iliyochukuliwa na halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Kakerege iliyotakiwa kulipwa mwaka 2017.

Inaelezwa kuwa kwa kipindi hicho walifanyiwa tathimini na kutakiwa walipwe fidia ya Sh.milioni 12.3 lakini halmashauri haikuganya hivyo.

Vilevile, wananchi wengine walilalamikia viongozi wa halmashauri hiyo kuwauzia viwanja na kushindwa kuwapatia viwanja vyao, huku wakichukua malipo ya viwanja hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu.

Akijibu kero hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Emmanuel Sherembi alieleza kuyatambua madai hayo na kueleza kuwa kama halmashauri tayari imetenga Sh.milioni 60 kwa ajili ya kulipa fidia hizo ambazo zitalipwa kidogo kidogo.

Kuhusu waliolipia viwanja bila kupatiwa viwanja vyao Mkurugenzi huyo aliwaomba radhi wahusika kutokana na usumbufu uliosababishwa na watumishi wa idara husika na kuagiza pale vitakapotangazwa viwanja vingine wapewe kipaumbele wananchi hao.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Bomboko alimuagiza Mkurugenzi huyo kuwaita wananchi hao wanaodai fidia ofisini na kupewa maelezo kamili juu ya kuwalipa fidia kwa wakati.

Kadhalika aliagiza TAKUKURU kuhakikisha wanafuatilia kwa kina baadhi ya migogoro ambayo imekuwa ikikwamishwa utatuzi wake kwa maslahi ya baadhi ya viongozi na kuwachukulia hatua stahiki watakaobainika kuhusika.

Kero nyingine zilizopokelewa ni pamoja baadhi ya wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kukatwa fedha zao kinyume cha sheria kwa kile kinachoelezwa kuwa ni makato ya kulima kwenye shamba la Kijiji.

Hivyo, Mkuu huyo wa Wilaya aliagiza kurejeshwa kwa fedha hizo haraka na agizo kutekelezwa hapohapo.




Ujumbe wa watumishi kutoka Wizara ya Madini, wakiangalia mradi wa maji wa Nyangoto, wilayani Tarime, uliotekelezwa na mgodi wa Barrick North Mara wakati walipofanya ziara ya kikazi mgodini hapo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# M/kiti CCM mkoa ageuka mbogo wizi vifaa vya ujenzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWENYEKI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, ameagiza kufanyike uchunguzi kuhusu wizi wa vifaa vya ujenzi wa Shule ya sekondari Ihugi iliyopo Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga.

Pia, ameagiza baada ya uchunguzi kufanyika wahusika watakaobainika wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wake wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi wa Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga na kuzitafutia ufumbuzi na kueleza kwamba watu wote wanaofanya ubadhilifu kwenye miradi ya serikali watashughulikiwa.

Alisema katika kero ambayo ameipokea ya wizi wa vifaa vya ujenzi katika shule hiyo imemkera, hivyo lazima aishughulikie haraka kwa kufanya uchunguzi ili kubaini watu wote ambao wamehusika katika wizi huo na wachukuliwe hatua kali na kuvitapika vifaa vyote.

"Rais Samia amekuwa akifanya ziara nje ya nchi kutafuta pesa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo na ujenzi wa shule hizi, lakini wanatokea baadhi ya watu na kuanza kuiba vifaa vya ujenzi, CCM Mkoa wa Shinyanga suala hili tunalishughulikia wote waliohusika watakamatwa tu,"alisema Mlolwa.

Aidha, aliwataka watu ambao wamekuwa wakihusika kwenye ujenzi wa miradi yote ya Serikali wawe wazalendo na nchi yao na kupenda maendeleo na kuacha kuifanyia hujuma, ili kero za wananchi zipate kutatuliwa na wanafunzi waache kusoma shule umbali mrefu.

Aliwahakikishia pia wananchi, kwamba kero zao zote ambazo wameziwasilisha kwenye mkutano wake na zingine tayari zimeshatatuliwa na wataalamu wa halmashauri ambao aliambatana nao.

Naye Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, akijibu kero za wananchi wa kata hiyo likiwamo suala la ukosefu wa maji na umeme alisema kwa mujibu wa TANESCO kupitia mradi wa REA, hadi kufikia Desemba mwaka huu umeme utakuwa tayari umewaka, huku suala la maji ndani ya muda mfupi yatafika kutoka Ziwa Victoria.

Awali baadhi ya wananchi wa kata hiyo waliwasilisha kero zao likiwamo suala la wizi wa vifaa vya ujenzi wa shule ya Sekondari Ihugi zikiwamo mbao na saruji, upungufu watumishi wa afya, maboma ya zahanati kutokamilika, ukosefu wa umeme, maji na ubovu wa miundombinu ya barabara.



Ukurasa 12

**UWEKEZAJI AWAMU SITA; BN. 6.7/- HADI BN.21.5/-...**

Mapinduzi bajeti yaiwezesha TARURA Manyara ukombozi madaraja na lami




Ukurasa 13

Hivi kwanini walimu wanastaafu?



Ukurasa 14

**Simulizi TASAF Pwani kuwasogezea milo mitatu, watoto wao kuingia chuo kikuu**

BUFE

IJUMAA OKTOBA 6, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Balozi Russia: Tuko vizuri na Samia, apiga 'polishi' urafiki tangu Nyerere

- Ushiriki wake kongamano lao na Waafrika
- Wavutiwa na uwazi wa milango uwekezaji

**Na Christina Mwakangale**



Balozi wa Russia nchini, Andrey Avetisyan, alipomtembelea, Rais wa Zanzibar, Dk, Husein Ali Mwinyi, Ikulu, Unguja, wakikabidhiana zawadi. **PICHA: MTANDAO**

KIHISTORIA kupatikana uhuru wa Tangayika na Zanzibar na hata baadaye, kuundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna historia ndefu ya ushirikiano kimaendeleo, pia urafiki na mataifa makubwa duniani.

Hiyo inafanyika huu ikisalia wastani wa wiki moja, kuadhimishwa kitaifa kumbukumbu ya Kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ambaye ndiye aliyesindika mzizi mkuu wa mafanikio hayo ya sasa, kwa upande wa Tanzania.

Tanzania mpya na mataifa ya Kiafrika baada ya uhuru, kwa muda mrefu zimekuwa zikijenga urafiki na mataifa hayo, ikiwamo Uingereza iliyowatawala, pia yale ya mrengo wa kushoto yakiwa katika itikadi ya kijamaa, kuendelea na safari ya ukombozi wao.

Daima urafiki huo wenye zaidi ya miongo sita sasa, bado haujaisha katika historia ya misaada ya kimaendeleo, kama ujenzi wa barabara na majengo ya huduma kama afya, nafasi ya elimu ikitanuliwa ndani ya nchi, pia fursa za ughaibuni.

Hapo ndipo yanatajwa mataifa kama China. Cuba na iliyokuwa Jamhuri ya Muungano wa Kisovieti (USSR) na hata baada ya kugawanyika, ipo Russia ya sasa na nyiginezo zinazoendelea kudumisha uhusiano huo.

Mfano hai, ni pale wakati USSR (katika nchi ya Russia), ilianzisha chuo kikuu ikikipa jina la cha Lumumba, umma mkubwa wa Watanzania wamenufaika kusoma na kurejea nyumbani, wakiwa na stadi za kutumikia nchi kitaalamu kama kwenye udaktari wa tiba na uhandisi.

Nchi ilikofikia sasa, inafafanuliwa na Russia kwamba serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ilipofungua milango ya ushirikiano wa kidiplomasia pamoja na ukuzaji uchumi kwa kukuza uwekezaji, imegusa ajenda nchi hiyo kuongeza ushirikiano na Afrika.

Balozi wa Russia nchini, Andrey Avetisyan, anaeleza kuwa Kongamano la Pili la Kiuchumi, liitwalo 'Russia-Afrika Summit' lililofanyika Julai mwaka huu, mjini St. Petersburg nchini humo lililenga kuboresha mahusiano yajayo.

Balozi wa Russia nchini, Andrey Avetisyan, anafafanua hilo Dar es Salaam, kwenye Kituo cha Utamaduni wa Russia-Tanzania (RTCC), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali, ya mwendelezo wa ushirikiano wao na Afrika.

Katika tukio hilo, Nipashe ilipata fursa ya kumuliza maswali Balozi Avetisyan, kupata ufafanuzi zaidi ya mustakabli huo, fuatilia maswali alioyoulizwa na Nipashe na namna alivyoyaoa ufafanuzi:

**SWALI: Kwa uzoefu wako, unaelezeaje wewe kukaa Tanzania, nini maoni yako kuhusu uongozi wa sasa?**

**JIBU:** Kwanza, napenda kushukuru kuwa hapa Tanzania ni nchi ya kwanza, ikiwa pia ni mara ya kwanza kufika barani Afrika. Sikuwahi kutembelea Afrika hapo awali.

Nimefurahi kukutana na Watanzania, wakarimu na tunafurahia Sera za Rais Samia za wageni kuja kuwekeza Tanzania na ndio miongoni mwa sera za Russia barani Afrika.

Kongamano lililofanyika St. Petersburg (alilohudhuria Rais Samia) nalo lililenga kukuza uhusiano na Afrika. Utayari wa Warusi kuja kufanya biashara Tanzania, unaendana na uhusiano ulioko katika mazingira ya uwekezaji.

Uhusiano wetu wa kisiasa pia umekuwa wa karibu zaidi tangu nyakati za harakati za ukombozi wa Tanzania chini ya Rais Nyerere (Mwalimu Julius), ambaye alikuwa rafiki wa nchi yangu. Tunaona fursa ambazo zinajengwa na sera za Rais Samia.

**SWALI: Ni kwa kiwango gani Tanzania na Afrika kwa ujumla wake, imeendelea kupokea nafaka kutoka Russia kipindi hiki cha mgogoro kati yenu na Ukraine?**

**JIBU:** Chini ya asilimia tatu pekee ya tani milioni 32.8, za usafirishaji zilizifikia nchi zenye mahitaji. Kwa ujumla, hakuna upungufu wa chakula duniani, isipokuwa zipo changamoto za usambazaji na si uzalishaji. Bei ya kimataifa ya nafaka inazidi kushuka, ikiwa imepungua kati ya asilimia nne hadi tano, mwezi Agosti.

Russia itaendelea kusafirisha chakula, pamoja na mbolea ili kuleta utulivu na athari zilizojitokeza duniani ikiwamo bei, kwa kuhakikisha upatikanaji wa hizo bidhaa. Tutahakikisha tunasambaza bidhaa zetu bure kwa wanaozihitaji.

Pia, mbolea kutoka Russia imekwishazifikia nchi ya Malawi na Kenya kwa usafiri wa meli tani 20,000 na itafika tani 34,000. Tunatarajia kutuma tani 23,000 nchini Zimbabwe na tani 34,000 Nigeria, hivi karibuni.

**INAENDELEA UK.12**

UCHUMI

UWEKEZAJI AWAMU SITA; BN. 6.7/- HADI BN.21.5/-...

# Mapinduzi bajeti yaiwezesha TARURA Manyara ukombozi madaraja na lami

- Ahueni ya Mfuko Jimbo; zamani misiba na kukwama mtoni
- Walikotoka zama za kuomba hifadhi, sasa madaraja kibao

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HADI sasa mkoani Manyara, barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), zinaleta mabadiliko ya tija kiuchumi na kijamii, kutokana na wepesi wa kusafiri na kusafirisha mazao, mifugo, mizigo na wagonjwa.

Meneja wa TARURA mkoa wa Manyara Mhandisi Salim Byaya, anasema tangu TARURA ianze mwaka 2017 mkoa huo umejenga barabara za lami kilomita 30.6, Changarawe kilometa 1,603.4 na zaidi ya kilometa 5000 ni za udongo, ambazo mtandao mzima ni zaidi ya kilomita 6759.

Meneja anasema, ni barabara zinazopitika hata kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli zao, huku serikali ya awamu ya sita imewaongezea katika mwaka wa fedha 2020/21, Sh. bilioni 6.7; mwaka 2021/22 Sh. Bilioni 17.08 na 2022/23 Sh. Bil. 21.5, akitaja ni ongezeko la asilimia 216.

Mhandisi Byaya anasema upande wa lami ulikuwa na kilomita 17.3 sasa hivi ni kilometa 30.6 sawa na ziada ya asilimia 76. Anakutaja Hanan'g kuna kilomita 1.82 za lami, Magugu mita 700 za lami na Orkesmet kilomita 1.85.

Ni kazi ya ujenzi anayoitaja kuwapo madaraja makubwa matatu, wakiwezesha yafike matano mkoa mzima. Pia, anataja madaraja makubwa yaliyojengwa ni: Dahaya katika barabara ya Masieda Mang'ola kwa zaidi ya Sh. Mil. 680, Bunyoda Sh. Mil. 839 na Daraja la Rugina, Sh. Bil. 1.19.

Katika hilo, anaorodhesha mafanikio ya kujengwa barabara za changarawe kutoka umbali wa jumla kilometa 904 mpaka kilometa 1603.4.

Byaya anasema, barabara mpya kwa miaka miwili wamefungua kutoka kilometa 2873.9 mpaka kilometa 3274.6, huku wakiwa na taa za barabarani 260.

Anasema mwaka huu wa fedha wataweka taa za barabarani Babati taa 68, Katesh taa nane na Mbulu taa 20.

Mhandisi Byaya anasema, katika mwaka wa fedha 2023/24, wametengewa zaidi ya Sh. Bil. 20.7 za kujenga kilometa 11.7 za Barabara za lami.

Katika kutuma kiasi hicho, Mhandisi Byaya anaahidi watafanya matengenezo barabara za changarawe kilometa 482, barabara za udongo kilometa 653.6, pia madaraja madogo na vivuko 125 kwa wilaya zote za Manyara.

Meneja anasema kwa mwaka huu, kuna Programu ya Benki ya Dunia (WB) ya kuondoa vikwazo, ikitengwa zaidi ya Sh. Bil. 2.8 kuhudumia mradi mmoja kwa kila wilaya.



Moja ya madaraja yanayojengwa mkoani Manyara. **PICHA: JALIWASON JASSON**

> **"Meneja huyo anaeleza kuwa biashara nyingi zitafunguliwa kati ya Mbulu na Dongobesh, kwani Dongobesh kulikuwa kama kisiwani, kwa kukosa mawasiliano ya barabara.**

### WANANCHI WALIVYOIPOKEA

Mkazi wa kijiji cha Orkine, kilichoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Dickson Isaya, anasema kujengwa Daraja la Orkine, kunawasaidia kusafirisha mazao kwenda sokoni wilaya jirani, kama Kongwa, Kibaigwa na Chamwino, pia Gairo mkoani Morogoro.

Isaya analitaja kuwa ni daraja lilorahisisha mawasiliano na shughuli za kibiashara na za kijamii, ambazo hazikuwapo.

Anasema kabla ilipokuwapo mvua, hawakuweza kufika ng'ambo ya pili kununua mahitaji, wakilazimika kusubiri maji yapungue mtoni, ndio wavuke au wanapokwama huko, wanaomba hifadhi kulala kwa majirani wakazi jirani na daraja hilo.

"Hapa wanafunzi walikuwa hawawezi kuvuka mvua ikinyesha mpaka wasubiri mvua iache au wanalazimika kutoenda shule,"anasema Isaya

Mkazi mwingine, Petro Salun, anaeleza namna kukosekana daraja kuliwapoteza ndugu zao zaidi ya saba, akiwamo mjomba wake aliyefika eneo hilo usiku amelewa.

Anasimulia alipojaribu kuvuka maji yalimsomba na walimuokota akiwa ameshapoteza maisha, sasa anaishukuru serikali kuwajengea daraja hilo, ikimaliza kero tajwa.

### TARURA / HALMASHAURI KITETO

Meneja wa TARURA wilayani Kiteto Mhandisi Edwin Magiri, anasema wilaya hiyo ina mtandao wa barabara kilometa 1300.75 na zilizohakikiwa ni kilometa 1200.

Anasema zaidi ya kilometa 200 ni changarawe, lami kilometa 2.8 na zinazobaki za udongo.

Kwa mujibu wa Mhandisi Magiri, kwa mwaka wa fedha 2022/23, wamejenga madaraja sita makubwa yanayosaidia kuondoa adha ya mawasiliano ya umma kufanya shughuli zao. Anataja madaraja yaliyojengwa na TARURA kuwa ni la Orkine Sh. Mil. 229.1; Dongo Sh. Mil. 136 na Njipa kwenda Ndiligi Sh. Mil. 117.

Anataja yaliyojengwa kwa mawe ni; Mwanya kwenda Kiperesa lenye midomo minne, Sh. mil. 110; Gifukuza Sh. mil. 116 na la Orkine Namba Mbili Sh. mil. 235.

Mtaalamu huyo wa barabara, anasema wananchi kijijini Orkine, ilipokuwa mvua ikinyesha, hawakuweza kuwasiliana na upande wa pili.

Analitaja kuwa la ukombozi kikazi, likiunganisha wilaya zilizotajwa kibiashara na wakazi za Kongwa, Chamwino na Gairo, ikibeba sura ya kiungo hadi Dar es Salaam.

Meneja huyo anakiri namna wanakijiji hicho walivyokwama kuvusha mazao yao, shida ambayo sasa imefutwa na daraja.

Katika hilo, anarejea malengo ya TARURA Manyara, barabara zake mpaka mwaka 2025 ziwe zinapitika kwa asilimia 85, akiahidi Kiteto watajikita kwenye madaraja, kurahisisha usafirishaji mazao ya wakulima.

Mhandisi Magiri anataja kikwazo chao ni wafugaji kupitisha mifugo kwenye barabara na wakulima kulima kwenye hifadhi za barabara.

Hapo anarejea Sheria ya Barabara mwaka 2007, ikitaka barabara za wilayani kuachwe mita 40 kila upande. Kwa sasa, sheria za wilayani hapo, zinaagiza faini ya Sh. 5000 kwa kila mfugo kupitishwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Kiteto Abdallah Mohamed, anaishukuru serikali kuwajengea barabara zao, akiitaja awamu ya sita kufanikisha azma hiyo.

"Kuna madaraja na barabara zilikuwa hazijafunguliwa toka uhuru, ila (Rais) Samia amezifungua hapa Orkine, watu wamekufa kabla ya kujengwa daraja,"anasema Mohamed.

Meneja wa TARURA wilaya ya Simanjiro Mhandisi Naftar Chaula, anasema wamejenga lami takriban kilometa mbili kwa Sh. Mil. 500, mradi uliokamilika Juni mwaka huu na mwaka huu wa fedha uliopo, 2023/24 watajenga kilometa moja ya lami kati ya Orkesmet na mji mdogo wa Mirerani, ukiwa na kilometa moja.

Mhandisi Chaula anasema katika eneo la Msitu wa Tembo ambalo lilikuwa korofi, wamejenga kilometa mbili za Barabara akitaja kwa awamu ya sita, serikali imewaongeza bajeti asilimia 200.

### JICHO LA MBULU

Meneja wa TARURA wilaya ya Mbulu, Mhandisi Nuru Hondo, anasema kata ya Bunyoda ilikuwa na shida ya mawasiliano ya barabara inayounganisha mikoa ya Arusha na Manyara, wamejengewa daraja la Bunyoda kwa Sh. Mil. 839, akilitaja eneo hilo lilikuwa halipitiki, sasa limefunguka kuinua uchumi wa jamii mahali hapo.

Meneja huyo anaeleza kuwa biashara nyingi zitafunguliwa kati ya Mbulu na Dongobesh, kwani Dongobesh kulikuwa kama kisiwani, kwa kukosa mawasiliano ya barabara.

Hondo anasema mwaka 2017, TARURA ilipoanza walikuwa wanapatiwa Sh. Mil. 300 kwa mwaka, ila sasa imepaa hadi kati ya shilingi bilioni tano na sita, fedha nyingi ni zao la tozo za Mfuko wa Jimbo.

Mkazi wa kijiji cha Bunyoda, Andrew Awee, anasema Daraja la Bunyoda linapitisha mazao yao na anaiomba serikali iendelee kutoa fedha za Barabara, akikumbusha kabla mahali hapo walivusha wagonjwa kwenda hospistali kwa machela.

### WANA -BABATI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Gichameda, Maliali Kesy, anasema kwa miaka mitano mpaka sita wameishi mfano wa kisiwani, kutokana na Mto Rugina kuharibu mawasiliano yao ya barabara.

Kesy anasimulia mikasa, namna mvua na mito zinapochachamaa kwa mafuriko, watu walikimbia makazi yao, huku mkazi Gichameda Eleso, anaeleza vijana walivyotembea na kaptula za kuvuka mito.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Babati Mhandisi Aloyce Nombo, anasema barabara ya Gichameda mpaka Magugu, ilikuwa haipitiki kabisa na eneo hilo lilikuwa la kilimo cha miwa, hivyo wananchi walishindwa kuisafirisha kwenda kwenye Kiwanda cha Manyara Sukari.

Nombo anasema TARURA wametumia Sh. bil. 1.1 kujenga madaraja makubwa mawili, ili kurahisisha mawasiliano hayo kwa wananchi.

Vilevile anataja wamejenga kilometa 9.4 kutoka Gichameda mpaka Magugu na yamejengwa madaraja madogo tisa, kusaidia kufungua fursa za kiuchumi kwa umma.

### KUTOKA HANANG'

Mwendesha bodaboda maarufu, Nicolaus Joseph, anaungana na hoja miundombinu imeboreshwa, akishauri serikali kujenga barabara zinazoelekea hospitali na vituo vya afya, zipitike kirahisi kunusuru wagonjwa na wahitaji kama wajawazito.

Meneja TARURA wilaya ya Hanan'g Mhandisi Paul Mlia, anasema wana mtandao wa barabara kilometa 1005.5 na ambazo ziko hali nzuri ni kilometa 243.6; hali ya nafuu kidogo kilometa 211.42, hali mbaya zikiwa na kilometa 595.48.

Mhandisi Mlia anasema maeneo mengi yalikuwa hayapitiki ila serikali ilipotoa fedha za tozo na mfuko wa jimbo zimesaidia barabara kupitika.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 wamejenga Barabara ya Gadafi mita 700 kwa kiwango cha lami kwa Sh. Mil. 499.

Aidha, anasema barabara za Changarawe Masakta na Maskaroda wamejenga kilometa 17 mwaka wa fedha 2021/22 kwa sh. Mil. 480.

Mlia anasema mwaka wa fedha 2023/24 watajenga kilometa 1.2 ya barabara ya lami na barabara za vumbi zitaendelea kuboreshwa ili zipitike.

### WABUNGE MANYARA

Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, anaishukuru serikali kutoa fedha za kujenga daraja la Gichameda, akikiri wananchi wake walikuwa kisiwani.

Pia, anataja daraja la Bacho linalounganisha kijiji cha Bacho na Isamu, ikiitarajiwa kizunduliwa Jumatatu ijayo, Oktoba 9.

Mwenyekiti huyo wa Bajeti wa Bunge la Tanzania, anasema kuna kazi zinaendelea barabara ya Riroda kwenda Duru inajengwa, Gidasi Bubu hadi Dudiye inajengwa na Secheda mpaka Ufana.

Aliyekuwa mbunge wa jimbo la Babati Vijijini, Vrajil Jituson, anaishukuru serikali kwa kutoa fedha za kujenga daraja la mto Rugina katika Kijiji cha Gichameda.

## Balozi Russia: Tuko vizuri na Samia, apiga 'polishi' urafiki tangu Nyerere

INATOKA UK.11

Kwa kuongeza, usafirishaji huu kwa njia ya meli ambao ni bure, utafikisha jumla ya tani 200,000 za ngano kuelekea Somalia, Afrika ya Kati (CAR), Burkina Faso, Zimbabwe, Mali na Eritrea, kabla ya mwaka huu kuisha.

Mpango huu ni mradi wa pamoja baina ya Russia, Uturuki na Qatar, kufikisha tani milioni moja za nafaka kutoka Russia na kufanyiwa uchakataji nchini Uturuki na kuzifikia bure nchi maskini.

SWALI: Nchini Russia, kulikuwapo chuo kikuu kiitwacho Lumumba, ambacho kililenga kuwafundisha viongozi wa Afrika. Je, kikoje hadi sasa na viongozi kutoka Afrika wanakifurahiaje?

JIBU: Bado chuo kipo na kilipewa jina la Lumumba, baada ya mwanaharakati wa ukombozi kutoka Afrika, Patrice Lumumba. Si kwamba chuo kipo tu, bali kimekuwa eneo kwa Waafrika na wengine kutoka nje,

Kinaendelea kuwa eneo la mafunzo na eneo muhimu kwa Waafrika na wengineo wageni kutoka nje, kusoma kwa fani tofauti. Namba ya wanaofika kusoma vyuo vya nchini Russia kutoka Tanzania kupitia ruzuku ya masomo inaongezeka na kufikia 19,000 mwaka huu, ila nina uhakika namba ya Waafrika itakuwa, kwa ajili ya kuja kusoma.

Ninahamasisha wanawake kwa wanaume wa Kitanzania kufika Russia na kusoma. Kila mmoja anajua ubora wa Russia katika elimu, madaktari wengi waliosoma Russia wanafanya kazi nzuri sasa Tanzania na si madktari tu hata wahandisi, taaluma yeyote ambayo inahitajika.

Wahitimu wanaweza kutufikia na kujadili nao namna ya kupata vyuo bora nchini Russia kulingana na mahitaji yao. Kipaumbele chetu kimojawapo ni katika elimu. Tunashawishi Watanzania wengi zaidi kutuma maombi, ili kujiunga na vyuo vilivyoko Russia.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hivi kwanini walimu wanastaafu?






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

TUMEKUWA tukiambiwa tunapambana na maadui zetu watatu; ujinga, umasikini na maradhi. Ni kweli maadui hawa walitusakama sana katika mazingira tulimoishi.

Na hawakuzaliwa leo au jana, bali ni tangu kuumbwa kwa dunia, wamekuwa wakituzingira na kutukwaza katika mambo yetu.

Hata hivyo, zamani hatukuwa tukipambana nao kwa fedha kama sasa. Zamani ujinga tulikabiliana nao kwa wazee kutuasa na kutuonya kuhusu mambo mbalimbali, ikiwamo pia kutuelekeza jinsi ya kukabiliana na matatizo yoyote hata kufanikiwa.

Walitufunza adabu na kuheshimiana.

Umasikini tulikabiliana nao kwa kuzalisha vyakula sisi wenyewe kwa nguvu zetu, tukipata chakula kwa kuchimba, kugema, kuangua na hata kubangua maganda ya miti.

Maradhi tulikabiliana nayo pia kwa kuchimba, kubangua na kuangua.

Tulichimba mizizi na kuichemsha au kuitafuna mibichi, kama ambavyo tulibandua magamba ya miti na kuchuma majani ya miti na kuangua matunda.

Hatukulazimika kutumia mitambo au mashine kupata mahitaji yote haya yaliyochangia kuendeleza maisha kama binadamu, hivyo hatukuwa na gharama ya kifedha, bali nguvu zetu wenyewe kujipatia hayo.

Tunasimuliwa jinsi binadamu walivyotengeneza mavazi kutokana na magome ya miti, lakini pia ngozi za wanyama waliouawa kwa ajili ya chakula na dawa.

Vyote hivyo vilipatikana bila malipo wala masharti, bali uwezo wa kila mmoja kuchimba mizizi, kubangua maganda ya miti, kuchuma majani na hata kuangua matunda, pia kuchuna na kuwamba ngozi.

Miaka ilivyozidi kwenda, ulimwengu ulibadilika, ndivyo polepole masuala ya gharama kifedha yakaingia katika kukabiliana na maadui hao, zikajengwa shule, zahanati na hospitali, pia biashara ikaanza.

Yote hayo yalianzishwa ili kukabaliniana na madui hao hao;ujinga, umasikini na maradhi. Serikali zilizoanzishwa, zikaunda wizara zilizoshughulika na maadui hao, hao watatu na wengine.

Kama ningebahatika kuwa Rais wa nchi au Taifa lolote, kipaumbele changu kingekuwa ni kwenye wizara tatu tu za msingi, ambazo ni

Elimu ili kukabiliana na ujinga, Afya kukabiliana na maradhi na Chakula, kukabiliana na umasikini.

Ukishakuwa na wizara hizi tatu, hizo zingine hazina ulazima kabisa, kwani mambo yote yanafanywa na watu wenyewe, tena bila ya gharama.

Lakini la msingi ni la afya. Binadamu akiwa mjinga, ujinga hauwezi kumwondoa duniani mara moja na akiwa masikini hali kadhalika, ingawa akikosa chakula kwa muda mrefu atapoteza maisha na akiwa dhaifu kiafya, ni rahisi kupoteza maisha.

Hivyo kwa mtazamo huu, tukilinganisha elimu na afya, bora kuwa na afya ili hayo mengine ya elimu na utajiri yatafutwe, kwa sababu tajiri au msomi asiye na afya ni mzigo tu kwa jamii, hakuna anachosaidia.

Elimu itawezesha wizara zingine zote kuendeshwa, chakula kitawapa nguvu wanaosimamia wizara hizo, lakini afya atakuwa ndiye mama wa kila kitu kwa kuwa ndiye anayewezesha mambo yote hayo kufanyika.

Kwa maana hiyo, kwa taifa kama Tanzania linalohimiza watu kulipia afya na elimu kutolewa bila malipo, bado linahitaji kubungua bongo, kwa sababu lina idadi kubwa ya masikini wasioweza kugharimia afya zao, matokeo yake wanapoteza maisha.

Hivyo basi, linatakiwa kubadili gia angani kwa elimu na afya kubadilishana, ili watu walipie elimu huku wakitibiwa bure na kuachana na malumbano na makongamano ya muda mrefu ya bima ya afya.

Hivi sasa watu wengi hususan vijana, wamepoteza mwamko wa elimu shuleni au vyuoni kama ilivyokuwa zamani, mtoto aliyefaulu na kusonga mbele kimasomo alifurahi, kwani alitarajia baada ya hapo kwa mfumo ulivyo, aajiriwe na kujisaidia na kusaidia wazazi wake kimaisha.

Vivyo hivyo, wazazi walikazania sana watoto wao wafaulu na kupata elimu ya juu kwa mustakabali huo huo, lakini hivi sasa, kuna wimbi kubwa la wasomi wasio na chochote wakijilaumu kupoteza muda madarasani na kuishia kurejea majumbani.

Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba amekuwa akilisemea hili, kwamba watoto wanapoteza miaka mingi shuleni na hatimaye hurejea kwa wazazi wao kufanya kazi zile zile walizofanya kabla ya kuanza shule.

Kwao ni upotevu wa muda na rasilimali fedha.

Lakini pia husema, ni nani aliyetafiti na kugundua, kuwa akili za mtoto zinahitaji kutumia mwaka katika darasa moja kama si kupoteza muda na rasilimali fedha?

Nami namuunga mkono, nikiuliza kama tunalia upungufu wa walimu shuleni katika mazingira ya sasa ya ujenzi wa shule nyingi na mwamko wa idadi kubwa ya watoto kujisajili, ni nani aliyetafiti akagundua kuwa mwalimu akishafikia umri wa miaka 60, anapoteza uwezo wa kufundisha?

Kwanini tunakubali walimu wastaafu, huku tukiwa hatuna walimu wa kutosha shuleni? Kwanini wasiombwe hao na kuwalipa posho kama mishahara na kama fedha hazipo, wabunge wakubali kupunguziwa mishahara wapewe?

Au tuanze kulipa ada, mishahara yao ipatikane. Mbona Rais Godfrey Binaisa wa Uganda (1979-1980) alipostaafu, alirudi kufundisha shule za msingi? Hivi mbona hatufikirii? Kila la heri!

UCHUMI

# Simulizi TASAF Pwani kuwasogezea milo mitatu, watoto wao kuingia chuo kikuu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA



Sehemu ya miradi ya wanufaika kutoka kaya masikini, wakijihudumia kwa biashara mkoani Pwani, inayotokana na mitaji ya TASAF. **PICHA: MAKTABA**

"FAMILIA yetu ilikuwa inategemea mlo mmoja, kuna wakati mwingine tunakula hatushibi, mimi na ndugu zangu tulikuwa tukiishi maisha duni.

"Ilifikia wakati kaka zangu watatu walikatisha masomo kutokana na hali ya nyumbani kupata chakula kwa shida, wote tukimtegemea mama pekee ambaye alikuwa anajishughulisha na kuuza mihogo shuleni, ambayo hata hivyo fedha aliyokuwa anapata haikukidhi mahitaji yetu," analalamika.

Huyo ni Siwema Chikawe, mkazi wa wilaya ya Mkuranga, mwanafunzi anayekwenda kuanza mwaka wa kwanza katika Chuo kikuu cha Dar es Salam, akikumbuka safari yake.

Anaelezea picha halisi ya maisha yao, kabla ya kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru kaya masikini, unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Siwema anaeleza, akiwa darasa la sita, ndio mama yake aliingizwa kwenye mpango huo na kuanza kupokea fedha kutoka TASAF, ambazo zilimsaidia kununua chakula na daftari. Anasema, mama yake, ndiye mlezi wa familia kutokana na baba yao kuwa na ulemavu wa macho, alikuwa akitumia fedha kidogo anayoipata kununua chakula, sambamba na kuanzisha bustani ya mboga kuongeza kipato.

"Tulizaliwa sita, watatu ndio walishindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni, waliendа kujitafutia maisha yao, tukabaki na wadogo zangu tukiendelea kumtegemea mama kwa kila kitu" anasimulia msomi huyo.

"Kuna wakati mama unamuona kabisa hana kitu, lakini alikuwa akitufariji kwamba tutapika chakula tu na sisi tulimuelewa, tulishazoea maisha yetu. Nilichokifanya ni kupambania ndoto zangu za kusoma kwa bidii, nije niwasaidie ndugu zangu" anaeleza.

**MAISHA YANABADILIKA**

Siwema anasema, kutokana na mama yake kuanza kunufaika na fedha za TASAF, akaona maisha yanabadilika na kuanza kula milo mitatu kama ilivyo kawaida kwa wengine.

Anasema, hali hiyo iliendelea na alipohitimu kidato cha nne, akafaulu kuchaguliwa kwenda kidato cha tano na fedha anayopata mama yake haikutosha kugharamia mahitaji.

"Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, na Ofisi ya Wilaya ya Mkuranga, walichanga na kuninunulia vifaa vya shule na ada, nikafanikiwa kwenda kusoma kidato cha tano na sita, mahitaji mengine mama akiendelea kugharamia" anaeleza.

Anasema kwa sasa anatarajia kwenda kuanza masomo ya chuo kikuu, huku mama yake akiendelea kuwa ndani ya mpango, lakini fedha anazopata hazikidhi kulipa ada.

"Nawaomba wadau wa maendeleo watakaoguswa wanisaidie kuanza masomo ya chuo, kwani pamoja na fedha mama anayoipata, bado haitoshelezi kumudu mahitaji ya ndugu zangu wanaosoma na mimi kukidhi gharama za chuo," anasema.

Naye, Subira Saidi, mkazi wa Kimbwanindi Wilaya ya Mkuranga, anaeleza kwamba hali ya maisha ya nyumbani kwao ilikuwa duni, kabla ya kuingizwa kwenye wanufaika wa TASAF.

Anataja, baada ya familia yake kuingizwa kwenye mpango huo, walibadilika na kuanza kula milo miliwi, huku unafuu wa vifaa vya shule ukianza kupatikana.

Pia, anataja kupitia TASAF, mama yake ameanzisha mradi wa kufuga kuku, unaowasaidia kujikwamua kutoka kwenye hali ya umasikini. Ni simuzi inayowagusa Ashura Omari kutoka kitongoji cha Mwembebaraza katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, akishukuru serikali kwa kuendeleza mfuko wa TASAF, kwa kuwa msaada mkubwa kwao jamii maskini.

**BOSI TASAF**

Akiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Meneja Ufuatiliaji wa TASAF, Salome Mwakigomba, anafafanua mradi ulivyo, akipiga marufuku fedha wanazopata kupitia mfuko huo, kuwa matumizi kama vile sherehe za kuwaozesha mabinti, tena wa umri mdogo.

Mwakigomba ametamka akiwa ziarani, akitembelea kitongoji cha Mwembebaraza akiwa na waratibu wa TASAF, na wahasibu kutoka halmashauri tisa za mkoa wa Pwani, ikiwa sehemu ya kujifunza maisha ya walengwa na walivyofanikiwa kwenye mradi Kilimo Mjini.

Mwakigomba, amewaeleza walengwa kuwa kazi ya fedha za TASAF ni kuziinua kaya maskini kutoka hali duni hadi unafuu, kiasi cha kuishi kwa kula milo mitatu kwa siku na kuhakikisha watoto wanaenda shule.

Anasema; "Serikali inafanya kazi ya kujenga miundombinu mbalimbali ya elimu ikiwamo kujenga madarasa, inatoa fedha kwa kaya maskini ili kuwawezesha watoto kusoma itakuwa jambo la kushangaza kama malengo ya mpango huo hayafuatwi.

"Acheni kutumia fedha za TASAFkuozesha watoto wa kike,waacheni wasome maana kuna tabia ya kuchukua elfu ishirini mara elfu themanini kuzipeleka kwenye sherehe za kuwaozesha mabinti ,hiyo sio sawa!"

Mwakigomba,anawasisitiza wazazi kuweka kipaumbele cha kuwasimamia watoto kusoma na waachane na tamaduni zilizopitwa na wakati.

**RC KUNENGE**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, anawakumbusha waratibu wa mfuko huo kuwafuatilia wanufaika na kuwatoa wale walioimarika, ili wengine wapate nafasi.

Kunenge pia, anawawataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wapya mkoani Pwani, kutoa kipaumbele kwenye utokomezaji umasikini kwenye maeneo yao, sambamba na kuwa na mfumo wa ufuatiliaji walengwa wa TASA, ikkiwa ndio njia sahihi ya kuifanikisha.

> **"Nawaomba wadau wa maendeleo watakaoguswa wanisaidie kuanza masomo ya chuo, kwani pamoja na fedha mama anayoipata, bado haitoshelezi kumudu mahitaji ya ndugu zangu wanaosoma na mimi kukidhi gharama za chuo.**

**MRADI UNAVYOENDESHWA**

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Pwani Roseline Kimaro, anasema Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, unatekelezwa katika Halmashauri tisa za mkoa Pwani zenye jumla ya vijiji 417 na hadi kufikia Juni 2023 kaya zinazonufaika na mpango ni 35,427.

Kimaro anabainisha idadi hiyo imepungua kutoka kaya 37,663 kwa takwimu za mwaka 2020/2021 kwa sababu mbalimbali, zikiwamo vifo na watu makazi na baadhi yao kutohudhuria uhakiki kwenye daftari la mpango huo.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, mpango unatekelezwa katika sehemu nne, ambazo ni miradi ya ujenzi wa miundombinu, mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya, Uhawilishaji fedha kwa kaya masikini (CCT) na programu ya miradi ya ajira za muda kwa kaya za walengwa, pia utoaji mafunzo kujenga uwezo.

"Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 sh. Biln 13.9 zilipelekwa katika madirisha matano na kulipwa kwa walengwa kwa njia ya taslimu, mtandao na kupitia wakala ambazo zimekuwa sababu ya walengwa kuongeza kipato cha kaya na kuwezesha uhakika wa chakula," anasema.

Kimaro pia anaeleza kwamba miradi ya kutoa ajira inatekelezwa katika Halmashauri nne ambazo ni Bagamoyo, Kisarawe, Chalinze na Kibaha.

Akizungumzia Mpango wa Kuweka Akiba na Kukuza Uchumi wa kaya, anasema mkoa kupitia halmashauri tisa, umefanikiwa kuunda vikundi vya kuweka akiba 1,478.

Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 sh. Miln 847.8 zimepokewa na walengwa 4,441 kwa ajili ya kuongeza mtaji na kukuza uchumi wa kaya na zimewajengea walengwa katika utunzaji rasilimali.

Mafanikio anayataja ni kuimarika kwa kuwa na uhakika wa chakula ikiwamo milo mitatu tofauti na ilivyokuwa awali mlo mmoja, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaohudhuria masomo ya shule za msingi, sekondari na chuo kikuu.

"Kabla ya mpango huu wanafunzi walikuwa hawapati mahitaji ya shule na sasa baadhi yao wametimiza ndoto zao , wanafunzi wa shule za msingi ni 18475 na 4806 wa Sekondari ambao wanahudumiwa na mpango kati yao 52 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vikuu," anasema

Mengine ni kuimarika kipato na kuondoa utegemezi kwa watu wenye ulemavu wanaohudumiwa na mpango ambao ni 10,070 wanaonufaika na ruzuku za wenye ulemavu.






Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, akimhudumia mteja kwenye ofisi za mfuko huo, jijini Dodoma juzi, wakati wa wiki ya huduma kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'NGOs kataeni fedha za wafadhili zenye masharti magumu'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeyataka mashirika yasiyokuwa ya kiserikali nchini (NGOs) kukataa fedha za ufadhili wa miradi yenye masharti magumu ambayo hayaendani na mila na desturi za kitanzania.

Msajili wa bodi ya urataibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Mwantumu Mahiza, alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye jukwaa la mwaka la mashirika yasiyokuwa ya kiserikali nchini.

Alisema moja kati ya vitu ambavyo vimejitokeza katika jukwaa hilo la mwaka ni masharti magumu yanayotolewa na baadhi ya wafadhili kwenye fedha za miradi ambayo hayaendani na mila na desturi za kitanzania.

"Kumekuwa na tatizo la masharti magumu kwenye fedha zinazotolewa na baadhi ya wadau ambayo mengine hayaendani na mila na desturi zetu hili hata Rais amekuwa akilisemea sana kama mtanzania lazima kutanguliza uzalendo mbele."

"Fedha unayoimboa ni kwa malengo gani na je lazima uiombe fedha yenye masharti magumu kama ina masharti ambayo hayaendani na mila zetu na tamaduni zetu achana nayo," alisisitiza Mahiza.

Mahiza alisema kutokana na hali hiyo mashirika ambayo yamekomaa yanaweza kutumia vyanzo vya ndani kujipatia fedha kwa ajili ya kuendesha miradi yao.

"Mfano mashirika ambayo tayari yameanza kufanya biashara wanaweza kwenda benki kukopeshwa lakini yanayotoa huduma yanaweza kupata fedha kwa kutumia vyanzo vya ndani," alisema.

Aidha, alisema hoja nyingine ambayo imejitokeza mara nyingi katika jukwaa hilo ni uwazi kwa mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi yao katika jamii.

Pia, alisema mashirika mengi hayafahamu namna ya kuomba fedha katika vyanzo mbalimbali vya ndani na nje, hivyo mengi yao hugombania chanzo kimoja.

"Mashirika mengi hayajui kuomba fedha sasa changamoto hii tumeichukua na kama serikali tutaandaa utaratibu wa kutoa elimu kwa mashirika yetu ili yaweze kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali na kuzitumia katika kutekeleza miradi mbalimbali kwenye jamii "alisema Mahiza

Hata hivyo, alisema akiwa kama mwenyekiti wa bodi ya uratibu wa mashirika hayo ataendelea kushirikiana na serikali kuzifanyia kazi kero mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ili wanapokutana mwakani zisijitokeze.

# TAKUKURU, DCEA zatakiwa kutoa elimu kwa jamii, shuleni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) zimetakiwa kutoa elimu kwa jamii pamoja na vilabu vya kupinga vitendo hivyo katika shule na vyuo ili kufikia malengo ya kukomesha vitendo hivyo nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salumu Hamduni alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizindua kampeni ya tokomeza rushwa na dawa za kulevya shuleni na vyuoni kwa watumishi kutoka taasisi hizo uliofanyika jijini hapa.

Mkurugenzi huyo aliwataka watumishi hao waliopatiwa mafunzo ya elimu kuhakikisha wanaishusha hadi ngazi ya chini kwa klabu za wapinga rushwa vyuoni, shuleni na kwenye jamii ili kukabiliana na vitendo hivyo vya matumizi ya dawa za kulevya na rushwa.

Alisema elimu hiyo waliyoipata anaamini itakwenda kuwakomboa kwa wale wanaojihusisha na vitendo hivyo ukizingatia kuwa imekuwa ikidhoofisha na kuleta madhara kiuchumi kijamii kisiasa pia na nguvu kazi ya taifa.

Alisema mafunzo hayo yakawe mkombozi katika kusaidia kuwaokoa wale wanaojihusisha na vitendo ambavyo pia vimekuwa vikisababisha kupoteza mapato, vifo na gharama kwa serikali katika kuwahudumia.

"Watumishi ambao mmepata mafunzo haya kwa taasisi hizi mbili mkaweze pia kubadilishana taarifa zitakazowawezesha kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya na mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa."alisema.

"Rushwa imekuwa kichocheo kikubwa cha kukua kwa dawa za kulevya hapa nchini na duniani kwa ujumla, hivyo ni mategemeo yetu mtaenda kuweka wigo mkubwa na nguvu ya pamoja katika kukabiliana na kudhibiti mapambano tatizo la biashara ya dawa hizo za kulevya,"alisisitiza.

Awali, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, alisema lengo la kuzikutanisha pande zote mbili ni kuwajengea uwelewa wa kudhibiti vitendo hivyo vya matumizi ya dawa za kulevya na rushwa ambavyo vimekuwa vikiathiiri ukuaji wa uchumi.

Aidha alisema hali hiyo itawawezesha kupitia nafasi zao kuwapunguza watumiaji wa dawa za kulevya na vitendo vya rushwa na hatimae kupatikana nguvu kazi zitakazokuwa na uzalendo na kuimarisha uchumi ya nchi.

# Watumishi NSSF wapewa angalizo vitendo vya rushwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAFANYAKAZI wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wametakiwa kutojihusisha na vitendo vya rushwa ili kutochafua taswira ya mfuko huo.

Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Singida, Dk. Mohammed Kilolile alitoa kauli hiyo jana kwenye hafla ya ufunguzi wa maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja iliyofanyika Ofisi za NSSF mkoani hapa.

Dk.Kilolile alisema rushwa ina madhara makubwa kwa mfuko huo na kwa kila mmoja wao na pia ni adui mkubwa wa haki na kuharibu sifa nzuri ya mfuko ambayo imejengeka kwa muda mrefu.

Alisema serikali inapinga rushwa kwa vitendo hivyo mfanyakazi yeyote takayebainika kujihusisha na rushwa atashughulikiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) kwa mujibu wa sheria.

Alisema mfuko huo umeweka utaratibu wa ndani wa kutoa taarifa dhidi ya watumishi wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na unashughulikia taarifa hizo kwa usiri ili kulinda utambulisho wa watoa taarifa hizo.

Naye, Meneja wa NSSF mkoani hapa, Oscar Kalimilwa alisema Wiki ya Huduma kwa Wateja ilianzishwa rasmi kimataifa mwaka 1984 kwa lengo la kutambua umuhimu wa huduma bora kwa wateja na juhudi za wafanyakazi wanaotoa huduma bora kwa wateja. Kalimilwa alisema katika kutambua umuhimu wa huduma bora na kazi kubwa inayofanywa na watumishi, mfuko umeandaa hafla hiyo ili kuwashukuru wateja kwa ushirikiano wanaotoa kwa mfuko na kuwapa hamasa, kutambua mchango mkubwa wanaoufanya katika kuwahudumia wateja wao na kuamsha ari miongoni mwao ili kuendelea kutoa huduma bora.

Naye, Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Mkoa wa Singida, Beda Mgonja alisema kauli mbiu ya huduma kwa wateja kwa mwaka huu isemayo, 'Team Work' inawapa faida kubwa kwani jambo hilo linawaondolea mambo mengi hata mtu akiwa na msongo wa mawazo huisha na hutoa huduma nzuri.





Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya Maendeleo TIB, Robert Ndaki (katikati), akikata utepe kuzindua wiki ya huduma kwa wateja 2023, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Wengine ni wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askari 'feki' wawili wakamatwa wakifanya unyang'anyi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewakamata watu wawili wakijifanya ni askari polisi wakiwa wamemkamata mwananchi mmoja na kumnyang'anya Sh. 700,000 na simu tatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema watu hao walikamatwa juzi wakiwa kwenye eneo la Stendi ya Tunduma katika mji mdogo wa Mbalizi wilayani Mbeya wakiendelea na majukumu yao.

Aliwataja watu hao walikuwa wakijifanya ni maofisa wa Jeshi la Polisi kuwa ni Juma Mapunda (47) na Said Mwanyika (27) wote wakazi wa Songea mkoani Ruvuma.

Alisema watu hao walikamatwa na askari polisi waliokuwa kwenye doria, ambapo waliwakuta wakiwa wamemkamata mwananchi aitwaye Meck Mpepo ambaye walimuweka chini ya ulinzi na wakamnyang'anya fedha na simu.

"Baada ya kuwakamata tuliwahoji watuhumiwa hawa ambao wamekiri kufanya matukio kadhaa ya utapeli katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma kwa kujitambulisha kuwa wao ni maofisa wa Jeshi la Polisi," alisema Kuzaga.

Katika tukio lingine, Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi, huku baadhi yao wakiwa wamezifungasha kwa mfumo wa biskuiti.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Blandina Silvester (25) mkazi wa Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Samson Samwel (23) na Bruno Zubery (30) wote wakazi wa Itumbi wilayani Chunya pamoja na Jofrey Omondi (25) ambaye ni mkazi wa Migori nchini Kenya.

Alisema watuhumiwa wote kwa pamoja walikutwa na bangi zenye uzito wa kilo 87 na gramu 60 na kwamba Omondi ambaye ni raia wa Kenye alikutwa na gramu 30 akiwa amezifungasha kwenye mifuko na kuzisafirisha kwenye basi.

Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo pia linawashikilia watu wengine watatu kwa tuhuma za kufanya ramli chonganishi kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Erick Sinkala (33) mkazi wa Sumbawanga mkoani Rukwa, Saidi Mihayo (41) na Amos Nyazandu (25) wote wakazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam ambao walikuwa wanafanya ramli hizo na kujipatia fedha.

Alisema watuhumiwa wamekuwa wakiwalaghai wananchi kwa kufanya kafara za kuwaua ndugu zao ili kuwa matajiri na kumiliki mali hali ambayo inachochea mauaji na uhasama miongoni mwa wananchi wa maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo.

Alisema watuhumiwa walipopekuliwa walikutwa na vitu mbalimbali ambavyo wanafanyia kazi zikiwemo dawa za kienyeji na makaratasi ambayo yametengenezwa kwa mfumo wa fedha aina ya noti ambazo ndizo walikuwa wanazitumia kudanganya watu.

"Tuliwakuta na mabunda 15 ya karatasi zilizotengenezwa mfano wa noti, chekeche moja ya kufanyia shughuli za uganga, dawa za kienyeji za aina mbalimbali ambazo walikuwa wameziviringisha kwenye magazeti, cheti cha uganga wa tiba asili pamoja na vipeperushi," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wananchi kufanya shughuli halali za kujiingizia kipato badala ya kufanya shughuli ambazo ni halamu kwa maelezo kuwa jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria.

# DC: Wanaume Njombe msikimbie kuhudumia familia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAUME wilayani Njombe Mkoa wa Njombe wametakiwa kutokimbia majukumu ya malezi kwa mtoto pamoja na kuachana na mila potofu kwa wanawake kutokula mayai wakidai atapata shida wakati wa kujifungua na kusababisha baadhi ya watoto kudumaa.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Wilaya Njombe, Kissa Kasongwa, wakati wa mkutano wa kinamama na Wiki ya Kampeni ya Lishe Bora Kata ya Lugenge Halmashauri ya Mji Njombe.

Kissa aliwaomba wananchi wa kata hiyo hasa wanaume kutumia muda mwingi katika kuhudumia watoto kutokana na baadhi ya wanaume kukimbilia mjini baada ya kupata fedha.

"Acheni mila potofu ambazo zimekuwa zikichangia watoto kudumaa kutokana na kukosa lishe bora, wapendeni watoto kwa kuwatunza vizuri" alisema Kissa.

Pia aliagiza kila kata iliyopo katika Wilaya ya Njombe kuhakikisha inaunda kikundi cha lishe cha wanawake 10 kwa ajili ya kufuatilia lishe.

Kwa upande wake diwani wa Kata ya Lugenge, Filoteus Mligo, amewaomba wananchi kuacha kutumia muda mwingi katika kazi na kusahau suala la malezi kwa mtoto jambo ambalo linasababisha kuongezeka kwa udumavu katika kata hiyo.

Mkazi wa kata hiyo, Roida Mgaya alimuomba Mkuu wa Wilaya kuwapa semina wanaume ambao wamekuwa wakiwapa kazi nyingi wanawake na kusababisha kushindwa kutekeleza malezi ya mtoto kwa wakati, huku wanaume wakipata fedha huondoka na kwenda mjini.

Kwa utafiti ambao imefanyika katika Halmashauri ya Mji Njombe asilimia 6 ya wakazi wake ndiyo wanaokula mayai.

# Ujenzi wa daraja warudisha tabasamu wakazi kata ya Mababu

**Na Nebart Msokwa**, KYELA

WAKAZI wa kata ya Mababu wilayani Kyela katika mkoa wa Mbeya, wamesema ujenzi wa Daraja la Mababu umesaidia kurejesha mawasiliano ambayo yalikuwa yanakatika mara kwa mara, hasa kipindi cha mvua ambacho eneo hilo huwa linafurika maji.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa daraja hilo na mbio za mwenge, wananchi wa kata hizo wamesema walipitia changamoto nyingi ikiwamo shughuli za uchumi kukwama.

Kaunda Mwiganju mkazi wa kata ya Mababu alisema kwa muda wa miaka mitatu walikosa mawasiliano na shughuli za kiuchumi ziliyumba baina yao na kata nyingine zinazowazunguka.

Amesema kupatikana kwa daraja hilo litarejesha uhusiano na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kuishukuru serikali kwa kutatua changamoto hizo.

"Biashara ya mpunga ni kama ilisimama kwa sababu tulibaki kwenye kata yetu bila mawasiliano na maeneo mengine, tunaishukuru serikali kwa kutatua kero hii," alisema Mwiganju.

Naye Elizabeth Faustine alisema wanafunzi waliokuwa wakitumia njia hiyo walikuwa wakipata changamoto ya kutembea umbali mrefu hivyo daraja hilo limekuwa mkombozi kwao.

"Kwa sasa tunaweza kutembea kata moja na nyingine, wanafunzi wataachana na kero ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na biashara zitaanza kuchangamka," alisema Elizabeth.

Akitoa taarifa za mradi huo kwa kiongozi wa mbio za mwenge, Kaimu Meneja wa TARURA wilayani Kyela, Mhandisi Kaimu Mtungata alisema daraja hilo limegharimu zaidi ya Sh. milioni 161.

Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru, Abdala Shaibu alisema wameridhishwa na mradi huo, akiomba wananchi kulilinda na kulitunza.

Alisema: "Tunahitaji usimamizi kwenye mradi huu, tumekagua nyaraka tumeridhika nayo, maelekezo tuliyotoa yazingatiwe tofauti na hapo sheria zitachukua mkondo wake kwani zipo taasisi zenye tabia ya kudharau".





# Makamu wa Pili wa Rais atoa hadhari mvua za El-Nino

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah amewataka wananchi kusafisha mitaro na maeneo wanayoishi, wavuvi kusikiliza vyombo vya habari ili kupata taarifa za mwenendo wa hali ya hewa.

Aliyasema hayo wakati akifunga Mkutano wa 12 wa Baraza la 10 la Wawakilishi na kutoa tahadhari hiyo kufuatia uwepo wa taarifa ya tahadhari kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa kwamba kuna uwezekano Zanzibar kupata mvua kubwa za el-nino

Hivyo, aliwataka wananchi wanaoishi mabondeni wachukue tahadhari mapema za kuhama katika maeneo hayo hatarishi ili kujilinda na maafa yasiyo ya lazima.

Katika kuendeleza na kukuza uchumi, Hemed alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na harakati za ujenzi wa barabara kuu na barabara za ndani Zanzibar.

Alitawaka wananchi kutoa ushirikiano kwa kampuni za ujenzi wa barabara hizo na kuendelea kuwa wastahimilivu wakati wa ujenzi wa barabara hizo kutokana na usumbufu unaojitokeza.

Aidha, alisema katika kuweka mazingira mazuri wafanyabiashara wakubwa na wadogo serikali inaendelea na ujenzi wa masoko katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

"Hatua hii inaenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM Ibara 228 ya kuweka haiba nzuri ya miji yetu na kukuza kipato cha wafanyabiashara wadogo na wakubwa na kutoa fursa kwa wananchi na taasisi mbalimbali kuwekeza katika masoko hayo"alisema.

Hemed aliagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuwasimamia wajenzi wa masoko hayo kuwa na ubora na kumalizika kwa wakati kwa mujibu wa mkataba.

Pia, alitaka hatua za kisheria zichukuliwe kwa makandarasi wasio heshimu mikataba yao na watendaji wa Serikali wanaohusika na uzembe kuzorotesha utekelezaji wa miradi hiyo.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah akizungumza wakati akiahirisha kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakazi Uwanja wa Ndege Pemba kujazwa 'manoti'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mchakato wa kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba umekamilika.

Imesema ujenzi wa uwanja huo kwa sasa upo katika ngazi ya mthamini mkuu wa serikali kwa hatua za malipo.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif Al-Wardi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua wananchi wangapi watahusika na kulipwa fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Alisema awali kazi ya kufanya tathmini imefanywa na kampuni binafsi na kuwasilisha taarifa zake serikalini.

Alisema tayari mtathmini mkuu wa serikali ameipokea taarifa hiyo kwa ajili ya kufanya ukaguzi na kuithibitisha kabla ya kuipeleka serikalini kwa ajili ya kufanya malipo.

Aidha, alisema baada ya kukamilika kwa utaratibu huo ripoti ya tathmini hutakiwa kutangazwa kwa wananchi na taasisi za umma kwa mujibu wa miongozo ya fidia na taratibu zake sambamba na kuwapa elimu wananchi kuwajazisha fomu maalumu kwa ajili ya malipo.

Hata hivyo alisema kiwango anacholipwa mwananchi hubaki kuwa ni siri kwa mujibu wa kanuni za malipo ya fedha pamoja na kuzingatia usalama wake ili kuepuka matukio ya uhalifu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ambao ni mkopo kutoka Benki ya Uingereza ya UKEF ambao ni sehemu ya mikakati ya kukifungua Kisiwa cha Pemba katika sekta ya anga na usafirishaji.

# Dk. Mwinyi: Bado kuna uhitaji wa uwekezaji uchumi wa buluu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar bado ina mahitaji makubwa ya uwekezaji kwenye sekta ya uchumi wa buluu kupitia utalii, uvuvi na ufugaji wa vifaranga vya samaki, Bandari, mafuta na gesi pamoja na sekta ya usafirishaji wa majini.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na mabalozi wateule waliofika kujitambulisha, kupokea nasaha pamoja na kuaga kuelekea vituo vyao vya kazi kwenda kuiwakilisha Tanzania kimataifa.

Rais Dk. Mwinyi aliwataka mabalozi hao kuzichangamkia fursa za uwekezaji huko kwenye vituo vyao vya kazi na kuzileta nchini ili kuiimarisha utalii wa Zanzibar ambao ni tegemeo kwa uchumi wa nchi unaochangia asilimia 30 ya pato la taifa.

Aliwataka mabalozi hao kuangalia zaidi soko jipya la utalii mbali na kutangaza utalii wa fukwe na urithi lakini pia kuangalia fursa mpya za utalii wa mikutano, michezo na uwekezaji ili kuitangaza zaidi Zanzibar na kuiingiza watalii wengi wa maeneo mengine ya dunia ikiwemo China ambayo ina watalii wachache Afrika.

Kuhusu sekta ya uvuvi na ufugaji wa samaki Rais Dk. Mwinyi aliwataka mabalozi hao kuitangaza zaidi fursa hiyo pamoja na kutafuta wawekezaji na masoko ya kilimo cha mwani ambapo Zanzibar inaongoza kwa kuzalisha mwani Afrika.

Pia, aliwataka mabalozi hao kuangalia fursa ya masoko ya bidhaa za Tanzania kwa ujumla ikiwemo mazao ya viungo.

Aidha, aliwaelekeza mabalozi hao kuzichangamkia fursa za fedha, mitaji na mikopo pamoja na kuimarisha ushirikiano mwema kwa nyanja zote zikiwemo elimu ili kubadilishana uzoefu baina ya Tanzania na mataifa wanayokwenda kuiwakisha huko duniani.

Aidha Dk. Mwinyi aliizungumzia fursa ya Bandari jumuishi kwa Zanzibar akisema kwa sasa inahitaji Bandari kubwa ili kukidhi mahitaji ya uchumi.

Akizungumzia suala la mafuta na gesi pamoja na sekta ya usafirishaji wa majini, Rais Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inahitaji uwekezaji mkubwa kwenye sekta hiyo ili kuimarisha sekta ya biashara na uchumi wake kupitia Bandari za Zanzibar, Pemba, Tanga, Dar es Salaam, Mtwata.

"Zanzibar inahitaji vyombo vya usafiri wa majini kwa safari za Pemba, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na kwengineko kama Msumbiji, Komoro na sehemu nyengine za visiwa zilizozungukwa na bahari kwa maeneo karibu, Uchumi wa Buluu umejikita kwenye maeneo mengi ya uchumi unahitaji wawekezaji" alisema.

Hata hivyo Rais Dk. Mwinyi aliwataka mabalozi hao kuendelea kuimarisha ushirikiano mzuri na kuimarisha ujirani mwema uliopo kwa watakaoiwakilisha Tanzania kwenye nchi jirani.

Akizungumza kwa niaba ya mabalozi wenzake, Balozi Khamis Mussa Omar anaekwenda kuiwakilisha Tanzania jijini Beijing, China alimuahidi Rais Dk. Mwinyi mbali na kuzichangamkia fursa za uchumi na uwekezaji kwenye vituo vyao vya kazi pia watakwenda kuboresha zaidi uhusiano na ushirikiano wa kidiplomasia.

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Chongolo ataka kasi ujenzi mabwawa

**Na Neema Hussein,** MLELE

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesisitiza maelekezo ya chama kuhusu ujenzi wa mabwawa mengi ya kuhifadhi maji ya mvua ili kutatua uhaba wa maji nchini.

Chongolo aliagiza hayo juzi alipotembelea mradi wa Bwawa la Maji Nsekwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani Katavi linalotarajiwa kutoa huduma kwa wananchi zaidi ya 68,000.

Alisema wakitenga mabwawa 100 kila mwaka, baada ya miaka 10 kutakuwa hakuna tatizo la uhaba wa maji nchini.

Katibu Mkuu alisema Sh. bilioni mbili zilizotumika katika mradi huo zilete matokeo makubwa zaidi, akiitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kuanza kufuga samaki katika bwawa hilo.

Alisema samaki hao watasaidia lishe kwa vijana na wananchi kwa ujumla, akifafanua: "Watu wa kilimo, haya maji yanaweza yakaratibiwa watu wakalima msimu wote, mnaweza kutengeneza kwa ajili ya matumizi ya binadamu, lakini pia kwa matumizi ya kilimo. Tunataka yawe mengi ambayo yanaleta faida chanya.



"Mwaka huu wenzetu Wizara ya Kilimo wana mabwawa zaidi ya 100, pia wana visima vingi sana na ninyi pelekeni kwenye mabonde mabwawa ili kurahisisha huduma ya maji na nyingine kwa binadamu."

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi wa bwawa hilo, Meneja wa RUWASA Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Charles Mengo, alisema mradi huo unatarajiwa kuboresha huduma ya upatikanaji majisafi na salama kwa vijiji 16 katika halmashauri hiyo.

Alisema bwawa hilo lina uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 2.8 na ujenzi wake ulianza kutekelezwa Agosti 3, 2018.




Baadhi ya wafanyakazi wa benki ya Exim, wakiwa katika matembezi kwenye mitaa ya Jiji la Dar es Salaam juzi, kuonyesha mshikamano kwa wateja ikiwa ni sehemu ya kampeni ya benki hiyo ya kusherehekea wiki ya huduma kwa wateja inayoendeshwa chini ya kaulimbiu ya "Nguvu ya Pamoja, Nguvu Yetu". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bobi Wine akamatwa akiwa ndani ya ndege

**KAMPALA,** Uganda

KIONGOZI wa upinzani nchini Uganda, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, amekamatwa na wanausalama wakati alipotua uwanja wa ndege akitokea nje ya nchi.

Chama kikuu cha upinzani nchini humo, Uganda National Unity Platform (NUP) kilisema kiongozi wake huyo alikamatwa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Entebbe akiwa ndani ya ndege.

"Amechukuliwa akiwa bado kwenye ndege na kupelekwa katika maeneo yasiyojulikana. Hadi muda huu hatujui yuko wapi," alisema katibu mkuu wa chama cha NUP David Lewis Rubongonya.

Katibu huyo aliwaambia waandishi wa habari kuwa hata yeye alizuiliwa katika kituo cha ukaguzi wa kiusalama katika barabara kuu ya Entebbe ili asiende uwanja wa ndege kumpokea.



Kabla ya Bobi Wine kurejea, polisi walisema msafara uliopangwa kumpokea uwanja wa ndege haukuwa halali.

Hatahivyo, gazeti la Daily Monitor limeweka ujumbe kwenye mtandao wa X na kumuonyesha mbunge Mathias Mpuuga akiwa na Bobi Wine nyumbani kwake Magere, wilaya ya Wakiso muda mfupi baada ya kukamatwa uwanja wa Entebbe.

Rais Yoweri Museveni ambaye amekuwa madarakani tangu 1986, amekosolewa kwa kutovumilia upinzani.

Bobi Wine amekamatwa mara nyingi na amekabiliwa na mashtaka mengi yakiwemo ya uhaini.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yalisema serikali kwa muda mrefu imetumia mashtaka ya uwongo kukandamiza upinzani. **BBC**

# Tanzania yahimizwa kujizatiti utalii tiba

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeshauriwa kujiandaa kwa ajili ya utalii wa tiba kutokana na ongezeko la watu wanaoingia kwa ajili ya huduma za matibabu kutokana na kuboreshwa kwa huduma za afya.

Akizungumza katika Mkutano wa Afya Tanzania (Tanzania Health Summit) uliofanyika jana katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Tiba Utalii, Dk. Asha Mahita alisema ili kufanikisha mpango huo, huduma za afya katika ngazi zote zinahitaji kuboreshwa.

"Tanzania tumeanza kupokea wageni wengi wanaokuja kufuata matibabu. Hii inaonyesha kuwa tayari nchi za Afrika zimeanza kutuamini katika huduma za afya.

"Ni muhimu sasa hospitali na watoa huduma za afya kuanza kufikiria kwa upana zaidi ili mwananchi au mgeni apate huduma katika mazingira bora na kwa wakati, yenye utaalam wa hali ya juu na kuhudumiwa kwa lugha nzuri yenye kumpa matumaini. Pia ni muhimu kuwekeza zaidi kwenye eneo la utoaji huduma bora kwani kitakachotuongezea sifa kama nchi ni huduma bora," alisema.

Aidha, Dk. Mahita alisema jitihada za serikali ikiwamo filamu ya The Royal Tour zimefungua milango kwa watalii wengi kuingia nchini. Alisema katika kuhakikisha kunakuwa na huduma bora, Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza chachu ya maendeleo katika sekta ya afya ndiyo maana Tanzania sasa imeanza kupokea sifa katika tiba utalii.

Dk. Caroline Damian , Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Afya, aliwasilisha mada ya Ubora wa Huduma za Afya katika Ngazi ya Msingi wa Utoaji Huduma za Afya na Mwelekeo wa wa wizara kuhakikisha huduma bora za Afya zinapatikana Nchini

Mkutano wa Afya Tanzania (Tanzania Health Summit) ndio mkubwa zaidi wa kila mwaka wa huduma za afya nchini na unavutia mamia ya washiriki binafsi na wa mtandao kutoka mfumo wa huduma za afya kujadili maendeleo kuelekea Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Mada zingine zilizotawala katika Mkutano huo ni Kushughulikia Ukosefu wa Usawa wa Afya ya Mtoto kupitia Ufadhili Endelevu. Wasilisho lake litachunguza vikwazo nchini Tanzania vinavyozuia upatikanaji sawa wa matibabu ya nimonia ya kuokoa maisha na kuchunguza masuluhisho yanayoweza kusaidia kupanua wigo.

Pia Mkutano huo ulitoa taarifa mpya kuhusu ahadi zilizotolewa na serikali katika kuongeza uwekezaji katika ufadhili wa afya endelevu ambao unapaswa kuongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa Watanzania na kuwezesha nchi kukabiliana na majanga yasiyotarajiwa kama vile UVIKO- 19.

## Odinga apinga Kenya kupeleka kikosi Haiti

**NAIROBI, Kenya**

KONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga ametilia shaka uamuzi wa nchi hiyo kuongoza ujumbe wa kulinda amani nchini Haiti , akitaja kama hatua mbaya zaidi kuchukuliwa na serikali.

Odinga, alisema hayo katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni nchini humo siku ya Alhamisi.

Alisema, mpango wa kupelekwa polisi nchini Haiti haukuwa kipaumbele cha Kenya, wakati nchi hiyo ya Afrika Mashariki tayari ina matatizo ya kutosha.

"Kabla hata hujafika Afrika, Haiti iko mlangoni mwa Marekani ambalo ni taifa lenye nguvu zaidi duniani. Je, ni jambo gani la kipekee kuhusu Kenya ambalo linachaguliwa kuongoza kikosi cha kimataifa nchini Haiti?" alihoji Odinga.

Kiongozi huyo alionya kuwa hali ya Haiti ni hatari, na kupanga kupeleka kikosi hicho kuna hatarisha maisha ya polisi wa nchi hiyo.

"Majeneza yanapoanza kuwasili hapa, ndipo tutajuta. Haiti ni hatari na kuna uwezekano polisi wetu wakakumbana na matatizo huko," alisisitiza. **BBC**

# SHIME ASISITIZA USHINDI U-20 WAKIIVAA DJIBOUTI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Bakari Shime amesema kikosi chake kinaendelea vyema na maandalizi ya kuelekea mechi yao ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Djibouti.

Tanzanite itaikaribisha Djibouti katika mechi ya kwanza itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex na marudiano yakifanyika kwenye uwanja huo Oktoba 11, mwaka huu.

**Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema wamejipanga imara kuwakabili wapinzani wao na anataka kuona wapata ushindi katika mchezo huo wa kwanza ambao wao watakuwa nyumbani.**

Shime alisema matarajio yake ni kutumia vyema uwanja wa nyumbani ili kuifanya mechi ya marudiano ambayo pia itafanyika Tanzania kuwa nyepesi na hatimaye kufikia malengo ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Maandalizi yanaenda vizuri na matarajio yetu tushinde mechi zote mbili, kupata nafasi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia, tunatamani kushinda mashindano yote yaliyopo mbele yetu na kucheza fainali zote," alisema Shime.

Aliongeza anaimani timu zote za wanawake zitafanya vizuri katika mashindano yaliyopo mbele yao ikiwamo kucheza fainali kutokana na ubora wa wachezaji walionao na wanaopeperusha bendera ya Tanzania.

"Ni jambo linalowezakana kwa timu zote kucheza fainali kwa sababu benchi la ufundi linafanya jukumu ya kuandaa timu kuwa bora na viongozi wa TFF (Shirikisho la Soka Tanzania ) wanafanya majukumu yao kwa kuwapa mahitaji yote muhimu," Shime alisema.

Kikosi cha Tanzanite kinaundwa na idadi kubwa ya wachezaji wa Serengeti Girls (U-17), ambao mwaka jana walishiriki fainali za Kombe la Dunia zilizofanyika India na Tanzania ilitolewa kwenye hatua ya robo fainali.

Tayari 'dada' zao Twiga Stars wamebakisha mechi mbili ili kupata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON 2024), zitakazochezwa nchini Ivory Coast.



Wachezaji wa Tanzanite wakifanya mazoezi ili kujiandaa kuivaa Djibouti katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia kwa Wasichana (u-20) itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

## *Pwani yageukia soka la wanawake*

**Na Beatrice Shayo,** KIBAHA

UONGOZI wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Pwani (COREFA), umeanzisha bonanza la soka la wanawake kwa wanafunzi wa Shule za sekondani lenye lengo na kuibua na kuendeleza vipaji vya mabinti, imeelezwa.

Mwenyekiti wa COREFA, Robert Munisi, alisema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wasichana wa shule mbalimbali za sekondari za mkoani humo na kuongeza anaamini bonanza hilo litasaidia kutimiza ndoto za wasichana wenye vipaji ambao baadaye wataisaidia nchi katika timu mbalimbali.

Munisi alisema moja ya kipaumbele cha COREFA ni kuinua soka la wanawake kwa sababu mabonanza hayo yatawaimarisha na yatasaidia wachezaji kubadilishana uzoefu.

Naye Mwenyekiti wa Soka la Wanawake mkoani humo, Mariam Songoro alisema mpira ni ajira na kwa sasa wanawake wana nafasi kubwa ya kupata fursa ya kucheza katika timu za ndani na nje ya nchi.

Songoro alisema soka ni ajira kama zilivyo ajira nyingine ambazo zinainua maisha ya watu hivyo wanatoa nafasi kwa mabinti hao kuonyesha uwezo wao.

" Huu ni mwanzo tu mabinti zangu bonanza hili litawanufaisha, kazi yenu kubwa ni kujituma uwanjani, kufanya mazoezi, kuwa na nidhamu ambayo itawafikisha kule mnapopataka lakini msisahau kusoma kwa bidii ili muwe na uwezo wa kuzungumza lugha mbalimbali mtakapoenda katika nchi za wenzenu kucheza soka," Songoro alisema.

## Timu zote Ligi zaruhusu mabao

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Yanga kupoteza mechi dhidi ya Ihefu SC kwa kuchapwa mabao 2-1, hatimaye timu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara sasa zimeruhusu nyavu zake kutikishwa hadi kufikia raundi ya nne.

Yanga ilikuwa ndiyo timu pekee haijaruhusu bao, lakini kipigo ilichokipata kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbeya juzi kimeondoka rekodi waliyokuwa nayo ya kutoruhusu nyavu wake kuguswa.

Msimu huu Yanga imepoteza baada ya kucheza mechi tatu ikishinda zote bila kuruhusu bao ilipoichapa KMC na JKT Tanzania mabao 5-0 kila moja, na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo.

Yanga na Azam zimeruhusu mabao mawili kila mmoja, huku Simba na Singida Fountain Gate nazo zikiwa zimeruhusu idadi hiyo hiyo ya magoli kabla ya mechi zao za jana.

Mashujaa FC ndiyo timu pekee iliyoruhusu bao moja tu mpaka sasa katika mechi zake tano ilizocheza, huku KMC ikiruhusu mabao mengi zaidi kuliko klabu nyingine yoyote, wavu wake ukiguswa mara nane katika mechi nne ilizocheza.

## Wasanii Bongo Flava kupamba OktobaFest 2023

**Na Frank Monyo**

TAMASHA la kudumisha Utamaduni wa Tanzania la maarufu OktobaFest linatarajiwa kufanyika Oktoba 21, mwaka huu jijini Dar es Salaam huku lengo lake likiwa ni kuikumbusha jamii umuhimu wa kukubali na kuheshimu utamaduni licha ya kuwapo na ulimwengu wa kisasa wa mabadiliko.

Katika tamasha hilo kutakuwa na maonyesho ya vyakula mbalimbali vya kitanzania, sanaa, mitindo na burudani kutoka wasanii wa Bongo Fleva.

Akizungumzia jijini jana, Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Anitha Msangi alisema OktobaFest linalenga kuunganisha utamaduni katika siku moja yenye furaha.

"Ni zaidi ya tamasha, ni safari inayolenga kusherehekea watu, bia, mitindo, sanaa, chakula, na ladha tamu za vyakula vya kitanzania," Msangi alisema.

Aliongeza katika tamasha hilo kutakuwa mapishi ya kitamaduni kutoka makabila mbalimbali pamoja na utamaduni wa mavazi, mitindo sambamba pamoja na kutoa nafasi kwa wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na wasanii chipukizi kujitambulisha kwa wadau.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN UNITED, MAN CITY VITANI

MANCHESTER United na Manchester City zitamenyana kuwania huduma ya winga wa Brighton, Kaoru Mitoma, 26, ambaye ni raia wa Japan ifikapo Januari. ***(Fichajes)***

### TEN HAG YUKO SALAMA

NAFASI ya Erik ten Hag kama Kocha wa Manchester United iko salama kwa siku zijazo, licha ya kuwa na msimu mbaya wa klabu hiyo. ***(Guardian)***

### HOJBJERG NJIA MOJA

KIUNGO wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28, anataka kuondoka Tottenham Hotspur ikiwa klabu hiyo haiwezi kumhakikishia kucheza katika kikosi cha kwanza, huku Juventus ikimtaka. ***(Gazzetta)***

### HALL AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA wanataka kumsajili winga wa New York Red Bulls Mmarekani, Julian Hall, 15, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester United, Manchester City, Real Madrid na Bayern Munich. ***(Standard)***

### DAVIES MAMBO MAZURI

KLABU ya Bayern Munich inatazamiwa kumpa mlinzi wa pembeni wa Canada, Alphonso Davies mkataba mpya ili kuzima nia ya Manchester City, Chelsea na Real Madrid ya kutaka kumsajili. ***(90min)***

### SANE KUONDOKA BAYERN

WINGA wa Bayern Munich, Leroy Sane, 27, huenda akaondoka katika klabu hiyo msimu ujao, huku Barcelona na Real Madrid zikielekea kwa mshambuliaji huyo wa Ujerumani. ***(Bild)***

### KAYODE ATAJWA ARSENAL

KLABU ya Fiorentina inatazamiwa kumpa beki wa Timu ya Taifa ya vijana ya Italia ya umri chini ya miaka 19, Michael Kayode mkataba mpya na Arsenal wanaonyesha nia ya kumtaka. ***(Calcio Mercato)***

### SANTOS ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inafuatilia kwa karibu hali ya kiungo wa kati wa Brazil, Andrey Santos, 19, huko Nottingham Forest na wanaweza kumkumbuka mchezaji huyo kutoka katika kipindi chake cha mkopo ikiwa hatapata nafasi ya katika kikosi cha kwanza. ***(Athletic)***

### WILLIAMS KUBAKIA ATHLETIC

KIUNGO wa Athletic Club na Hispania, Nico Williams, 21, anakaribia kufikia kusaini mkataba mpya na kumaliza matumaini ya Brighton na Aston Villa kumsajili. ***(Sport)***

### TONEY KUONDOKA BRENTFORD

MSHAMBULIAJI wa England, Ivan Toney, 27, anafikiria kuondoka Brentford ifikapo Januari, huku Tottenham Hotspur au Chelsea zikitarajiwa kumnunua mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### TIMBER AINGIA SOKONI

ARSENAL, Liverpool na Manchester United ni miongoni mwa baadhi ya klabu za Ligi Kuu England zinazomwania kiungo wa kati wa Feyenoord na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Quinten Timber, 22. ***(90 min)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MOROCCO RASMI KUANDAA KOMBE LA DUNIA 2030

**NYON,** Uswisi

● ● ● Itashirikiana na nchi nyingine tano ikiwa ni mara ya kwanza...

MOROCCO, Hispania na Ureno zitakuwa mwenyeji wa fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2030, lakini mechi tatu za kwanza zitachezwa Uruguay, Argentina na Paraguay ikiwa ni kwa ajili ya kusherehekea miaka 100 tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo.

**Nchi hizo tatu zilitarajia kuandaa mashindano hayo kwa ujumla wake, ambapo yatachezwa zaidi Ulaya na Afrika Kaskazini – ikiwa ni michuano ya kwanza kufanyika katika mabara mengi.**

Sherehe za ufunguzi zitafanyika Morocco, Hispania na Ureno huku sehemu iliyosalia ya michuano hiyo ikichezwa katika nchi hizo tatu, baada ya Uruguay, Argentina na Paraguay kucheza mechi za ufunguzi.

Nchi zote sita zinafuzu moja kwa moja kucheza fainali hizo za 2030 na itakuwa ni mara ya kwanza kwa Morocco kupata nafasi hiyo baada ya majaribio matano ya hapo awali kushindwa.

Ureno pia watakuwa wenyeji kwa mara ya kwanza, huku wakishindwa kupata nafasi hiyo mwaka 2018 na 2022, lakini Hispania ina historia ya kuandaa michuano hiyo mwaka 1982. Argentina ndio mabingwa wa Kombe la Dunia kwa sasa baada ya kuifunga Ufaransa kwa penalti katika fainali ya kusisimua iliyochezwa mwishoni mwa mwaka jana.

Ushindi ambao ulimfanya Lionel Messi kushinda tuzo ya kifahari zaidi ya kandanda ya kimataifa baada ya kushindwa katika fainali ya mwaka 2014 dhidi ya Ujerumani.

Kwa kuzingatia sera ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), ya mzunguko wa mabara, ofa kutoka Shirikisho la Soka la Asia (AFC) na Shirikisho la Soka la Oceania (OFC) huenda zikazingatiwa kwa mwaka 2034.

Kabla ya furaha kuanza katika mabara mengi, mwaka 2026 fainali za Kombe la Dunia zitaandaliwa kwa ushirikiano wa pamoja wa nchi tatu ambazo ni Canada, Mexico na Marekani.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,159,5

MECHI KALI
TANZANIA PRISONS
VERSUS
SIMBA SC
1 | 7.91
X | 4.45
2 | 1.35

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Noel Makopo - 0652 952 XXX
2. Richard Richard - 0654 453 XXX
3. Alex Kalinga - 0655 146 XXX
4. Dlocle Bagenzi - 0656 295 XXX
5. Castor Deus - 0658 100 XXX
6. Baraka Daniel - 0675 368 XXX
7. Frank Tausi - 0718 891 XXX
8. Isaya Peter - 0719 316 XXX
9. Asha Njumba - 0719 355 XXX
10. Christina Christina - 0719 530 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ENRIQUE AKUBALI LAWAMA PSG IKIANGUSHWA ULAYA

**NEWCASTLE,** England

KOCHA, Luis Enrique alisema alaumiwe yeye kwa kichapo kizito cha mabao 4-1 ilichokipata Paris Saint-Germain kutoka kwa Newcastle United kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi.

PSG walizidiwa nguvu na vijana wa Eddie Howe kwenye dimba la St James' Park, huku Kylian Mbappe na wachezaji wenzake wakijikuta hawana la kufanya.

Shinikizo tayari linaongezeka kwa bosi huyo raia wa Hispania baada ya kushinda mechi tatu pekee kati ya saba za kwanza za Ligue 1 tangu kuteuliwa kwake msimu huu wa joto na kipigo hicho kitazua maswali zaidi.

Alipoulizwa katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo kama kushindwa huko lawama atupiwe yeye, Enrique alisema: "Ndiyo, kabisa. Hakuna shaka kuhusu hilo.

"Mimi ndiye mtu wa kwanza kuwajibika kwa hilo. Ninawajibika.

"Matokeo ya mchezo yalikuwa ya haki. Nadhani wachezaji wangu walitatizika kidogo na mchezo wao wa Newcastle. Walifanya kila kitu nilichowaomba wafanye. "Kwa utu na mtazamo, niliona ni nzuri lakini bila shaka tulifanya makosa ya kizembe ambayo yalisababisha mabao yao.

"Unapocheza kwa kiwango hiki huwezi kufanya hivyo."

PSG sasa inawafuata Newcastle katika nafasi ya pili katika kundi lao la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Enrique hakuona haja ya kuwa na hofu bado, akipendekeza ukali wa matokeo ulikuwa kwa upande wake.



## Xavi afurahia ushindi wa Barca

**LISBON,** Ureno

XAVI Hernandez amesema Barcelona iliondoa mzimu wao mbaya kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya bao la Ferran Torres kuwapa ushindi mwembamba wa 1-0 dhidi ya FC Porto hapo juzi.


Barca waliondolewa katika hatua ya makundi katika misimu miwili mfululizo iliyopita na wamekumbana na vipigo vikali katika mashindano hayo katika miaka ya hivi karibuni, hasa ugenini.

Ilibidi wajichimbie kwa kina kwa Porto, ambao walipata penalti ya kipindi cha pili na ikataliwa na VAR na bao lililokataliwa kuwa la kuotea, lakini wakapata ushindi uliowafanya wafikishe pointi sita baada ya michezo miwili.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri, lakini hatukuwa na udhibiti katika kipindi cha pili na tukateseka," alisema Xavi, ambaye hiyo ilikuwa ni mechi yake ya 100 kama Kocha wa Barcelona.

"Hii ni Ligi ya Mabingwa Ulaya na ni ngumu. Ni Ulaya, Porto ugenini... ni ngumu. Kila mtu alifanya kazi kwa bidii. Tunapaswa kuboresha, na tutafanya hivyo, lakini ni pointi tatu za dhahabu.

"Kulikuwa na mazungumzo kabla ya mchezo kuhusu mzimu (kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya) na tumewaondoa baadhi yao, na kuishinda timu kubwa ya Ulaya kwenye uwanja wao.



574,731/-

# GEITA GOLD FC YATAMBA KUENDELEZA KILIO YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya burudani na michezo SportPesa imeipongeza Yanga kwa kufanikiwa kuingia hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wametinga hatua ya makundi baada ya kuwaondoa Al Merrikh ya Sudan kwa jumla ya mabao 3-0.

Akizungumza kutoka makao makuu ya ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SportPesa, Abbas Tarimba amewapongeza wachezaji na viongozi wa Yanga kwa kufanikiwa kuingia hatua hiyo katika michuano ya msimu huu ambayo bado inaendelea.

"Sisi tukiwa wadhamini wakuu tunafarijika kuona mafanikio ya timu ya Yanga kwa jinsi inavyopiga hatua kubwa katika soka la Tanzania na kimataifa," alisema Tarimba.

Bosi huyo aliongeza wanaitakiwa mafanikio zaidi Yanga katika mechi zake zinazofuata na wanaamini wataendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Tunawatakia kila la heri kwenye mechi zijazo za hatua ya makundi katika kuipeperusha bendera ya Tanzania. Tunawapongeza viongozi wakiongozwa na Rais Hersi Saidi na pia wachezaji wote," Tarimba alisema.

Aliongeza SportPesa itaendeleza juhudi zake katika kuunga mkono, kuipa thamani na kuinua sekta ya michezo Tanzania.




Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati mwenye koti jeupe) akiwa na nyota wa zamani wa Taifa Stars ambao walihudhuria sherehe ya makabidhiano ya Sh. milioni 500 zilizotolewa na Rais, Samia Suluhu Hassan kwenda kwa Stars. **PICHA: TFF**

## Gamondi afunguka walipokosea

INATOKA UK. 24

mechi yao ijayo, tunakwenda kurekebisha makosa na kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo mwingine ambao tutaenda ugenini," aliongeza kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila alisema aliingalia Yanga namna wanavyocheza na kuwaandaa wachezaji wake kuwakabili na anawapongeza kwa kutimiza majukumu aliyowapa kabla ya mechi hiyo.

Katwila alisema alifahamu sehemu ambazo ni imara na kuandaa mbinu za kuziba njia zao na kwa kiasi kikubwa walifanikiwa.

"Haikuwa mechi rahisi, tulicheza kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu sana Yanga na kutumia makosa yao kupata alama tulizokuwa tunahitaji, niliwapa tahadhari kubwa wachezaji wangu kuhusu ubora wa safu ya ushambuliaji ya Yanga, tulifanikiwa kubana katika maeneo yao na kuzuia njia zote za kupata ushindi.

Mabadiliko ya kikosi pia yamenisaidia kwa sababu kuna wachezaji , Saadun (Nassor) na Never Tigere walianzia benchi mechi iliyopita lakini leo (juzi), nimewaanzisha ili kutafuta ushindi baadaye niliwatoa na kuwaweka wengine kwa lengo la kuimarisha safu yangu ya ulinzi baada ya kuona washambuliaji wangu wamefanya kazi vizuri ," alisema kocha huyo.

## *Simba yapaa kileleni kibabe*

INATOKA UKURASA 24

pigwa na Ntibazonkiza, penalti hiyo ilitokana na kipa, Amosi kumchezea madhambi, Moses Phiri, aliyekuwa ameingia uwanjani kuchukua nafasi ya Bocco.

Wakati huo huo Singida Fountain Gate FC imepata ushindi wake wa kwanza msimu huu baada ya kuwafunga wenyeji Mtibwa Sugar bao 1-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex jana.

Ushindi huo umeifanya Singida Fountain Gate ifikishe pointi tano na kupaa hadi nafasi ya nane kwenye msimamo lihi hiyo ya juu nchini.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Geita Gold kuikaribisha Yanga wakati Simba itawafuata Singida Fountain Gate keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/10/23 | 19:30 | Mallorca vs Valencia | 2.45 | 3.05 | 2.90 |
| 02. 07/10/23 | 19:30 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.70 | 3.65 | 2.29 |
| 03. 07/10/23 | 22:00 | Reims vs Monaco | 2.60 | 3.55 | 2.42 |
| 04. 08/10/23 | 15:15 | FC Lugano vs Servette Geneva | 2.12 | 3.45 | 2.80 |
| 05. 08/10/23 | 16:00 | Frosinone vs Verona | 2.26 | 3.30 | 3.00 |
| 06. 08/10/23 | 16:00 | Lazio vs Atalanta | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 08/10/23 | 16:00 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.80 | 3.40 |
| 08. 08/10/23 | 16:00 | GIF Sundsvall vs IK Brage | 2.48 | 3.20 | 2.48 |
| 09. 08/10/23 | 16:00 | Brighton vs Liverpool | 2.80 | 3.80 | 2.18 |
| 10. 08/10/23 | 16:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 3.30 | 3.40 | 2.07 |
| 11. 08/10/23 | 16:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.55 | 2.14 |
| 12. 08/10/23 | 17:30 | Lausanne-Sport vs FC Luzern | 2.44 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 08/10/23 | 17:30 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 14. 08/10/23 | 18:05 | Lens vs Lille | 2.15 | 3.45 | 3.05 |
| 15. 08/10/23 | 18:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.70 | 3.35 | 2.43 |
| 16. 08/10/23 | 18:30 | Hammarby vs Hacken | 2.35 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 08/10/23 | 19:30 | Alaves vs Betis | 2.75 | 3.10 | 2.55 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 06/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 03:30 | 5966 | Palmeiras vs Boca Juniors | 1.62 | 3.39 | 5.31 |
| 14:00 | 3927 | Llb Amasipiri FC vs Flambeau DU Centre | 4.39 | 3.27 | 1.77 |
| 15:00 | 2418 | Arema vs Pusamania Borneo | 3.84 | 3.48 | 1.78 |
| 15:00 | 2497 | Lamphun Warrior vs Ratchaburi | 2.68 | 3.13 | 2.40 |
| 15:00 | 3448 | Polissya Zhytomyr vs Dynamo Kiev | 4.96 | 3.64 | 1.58 |
| 15:00 | 3717 | KK Homeboyz vs FC Talanta | 1.70 | 3.71 | 4.12 |
| 15:00 | 4071 | Tusker vs Shabana FC | 1.44 | 3.99 | 6.47 |
| 15:00 | 5720 | Posta Rangers vs Nzoia United | 2.50 | 2.84 | 2.87 |
| 16:00 | 2155 | Uthai Thani FC vs Port FC | 3.80 | 3.54 | 1.77 |
| 16:00 | 3940 | Kitayosce FC vs Dodoma FC | 1.91 | 3.02 | 4.26 |
| 16:20 | 3929 | AL Bataeh (UAE) vs AL Khaleej Khor Fakkan | 2.34 | 3.39 | 2.58 |
| 16:20 | 5538 | Ittihad Kalba vs Hatta Club | 1.56 | 3.93 | 4.64 |
| 16:30 | 4346 | Magara Young Boys vs Inter Stars | 5.08 | 3.91 | 1.54 |
| 17:45 | 2519 | CS Constantine vs JS Saoura | 1.79 | 3.20 | 4.37 |
| 17:45 | 5612 | MC Alger vs ES Setif | 1.56 | 3.46 | 5.91 |
| 18:00 | 3543 | Al Nasr Riyadh vs Abha | 1.11 | 8.59 | 18.86 |
| 18:30 | 1548 | Zbrojovka Brno vs Pribram | 1.52 | 3.93 | 5.04 |
| 19:00 | 1108 | Velez Mostar vs NK Posusje | 1.57 | 3.66 | 5.29 |
| 19:00 | 2363 | Baniyas vs AL Wahda Scc (UAE) | 3.79 | 3.53 | 1.78 |
| 19:00 | 2725 | Al Hala Muharraq vs Najma Manama | 2.25 | 3.10 | 2.80 |
| 19:00 | 5568 | Coastal Union vs Azam | 4.37 | 3.38 | 1.77 |
| 19:00 | 5746 | Al Shabbab vs Al Hidd Club | 2.64 | 3.10 | 2.50 |
| 19:00 | 5817 | Farco FC vs Ceramica Cleopatra | 2.78 | 2.83 | 2.68 |
| 19:30 | 2669 | Empoli vs Udinese | 2.98 | 3.34 | 2.41 |
| 20:00 | 2728 | Alanyaspor vs Fatih Karagumruk | 1.98 | 3.40 | 3.50 |
| 20:00 | 4823 | Santa Clara vs Viseu | 1.91 | 3.28 | 3.74 |
| 20:00 | 4888 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 1.99 | 3.62 | 3.26 |
| 21:00 | 2092 | Helmond Sport vs Jong Utrecht | 1.72 | 3.83 | 3.98 |
| 21:00 | 2217 | Rapid Bucuresti vs FC Politehnica Iasi | 1.51 | 4.01 | 5.56 |
| 21:00 | 3119 | Jong PSV vs Maastricht | 2.06 | 3.74 | 2.92 |
| 21:00 | 3215 | Emmen vs Telstar | 1.47 | 4.31 | 5.54 |
| 21:00 | 3941 | Jong Ajax vs VVV Venlo | 2.55 | 3.63 | 2.34 |
| 21:00 | 4176 | Den Bosch vs FC Eindhoven | 2.67 | 3.28 | 2.41 |
| 21:00 | 4315 | Al Ittihad Jeddah vs Al Ahli Jeddah | 2.00 | 3.72 | 3.31 |
| 21:00 | 4992 | ADO Den Haag vs FC Oss | 1.47 | 4.31 | 5.54 |
| 21:00 | 5149 | Roda Kerkrade vs Jong AZ Alkmaar | 1.58 | 3.93 | 4.80 |
| 21:00 | 5229 | NAC Breda vs Groningen | 2.86 | 3.58 | 2.15 |
| 21:00 | 5921 | Dordrecht vs Cambuur | 3.07 | 3.69 | 2.01 |
| 21:00 | 5978 | FC Volendam vs Utrecht | 3.97 | 3.97 | 1.71 |
| 21:30 | 1905 | Monchengladbach vs Mainz | 2.07 | 3.75 | 3.34 |
| 21:45 | 1196 | Larne vs Crusaders Belfast | 1.67 | 3.63 | 4.23 |
| 21:45 | 2759 | Cardiff Met Uni. vs Barry Town FC | 1.83 | 3.34 | 3.79 |
| 21:45 | 3386 | Lecce vs Sassuolo | 2.46 | 3.54 | 2.77 |
| 21:45 | 4991 | Drogheda Utd vs Derry City | 4.63 | 3.83 | 1.58 |
| 21:45 | 5881 | Shelbourne vs Dundalk FC | 2.15 | 3.12 | 3.07 |
| 21:45 | 5971 | Linfield Belfast vs Glentoran Belfast | 1.75 | 3.52 | 3.92 |
| 22:00 | 2181 | Strasbourg vs Nantes | 2.19 | 3.34 | 3.39 |
| 22:00 | 3791 | Athletic Bilbao vs Almeria | 1.41 | 4.92 | 7.39 |
| 22:00 | 3806 | Aberystwyth Town vs Gap Connahs Quay | 7.26 | 5.24 | 1.28 |
| 22:15 | 3928 | Moreirense vs Boavista | 2.13 | 3.32 | 3.17 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 6, 2023

Nipashe




Xavi afurahia ushindi wa Barca UKURASA 22



Nahodha wa Simba, John Bocco (kulia), akifunga bao la pili katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya jana. Simba ilishinda mabao 3-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba yapaa kileleni

## ●●● Ni baada ya kuichapa Prisons, Singida FG yatakata...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matatu yaliyofungwa na Mzambia Clatous Chama, nahodha John Bocco na Mrundi Saido Ntibazonkiza yameiweka Simba kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kuirarua Tanzania Prisons mabao 3-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya jana.

**Simba imestarehe kileleni kwa tofauti ya pointi mbili juu ya Azam yenye pointi 10 ambayo ililazimishwa suluhu ya bila kufungana dhidi ya Dodoma Jiji Jumanne iliyopita wakati Yanga ambao juzi walipata kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Ihefu SC wako katika nafasi ya tatu na pointi tisa kibindoni.**

Haikuwa mechi rahisi kwa Simba ambayo ilianza kutanguliwa bao, lakini ilifanikiwa kusawazisha na kufunga mengine mawili yaliyofanya walipize kisasi cha kufungwa na Maafande hao katika mechi ya msimu uliopita.

Mchezaji aliyekuwa katika kiwango cha juu kwenye mchezo wa jana, Kibu Denis dakika ya nne tu alianza kulitia msukosuko lango la Prisons kwa kuwahadaa mabeki wa timu hiyo kabla ya kuachia shuti kali lililodakwa vyema na kipa, Amosi Yona.

Prisons ilijibu shambulio hilo dakika tano baadaye kupitia kwa Jememiah Juma alipoupata mpira katikati ya uwanja na kuwakokota mabeki wa Simba, nje kidogo ya eneo la hatari na kutandika mashine iliyotoka kidogo nje la lango.

Juhudi za Prisons za kufanya mashambulizi zilizaa matunda dakika ya 11, ilipoandikisha bao la kuongoza lililowekwa kwenye kamba na Edwin Balua, mfungaji aliupiga mpira wa faulo uliokwenda moja kwa moja wavuni kupitia kwenye maungio ya mwamba wa juu na wa pembeni, licha ya juhudi za kipa wa Simba, Ally Salim kuufuata bila mafanikio.

Faulo hiyo ilitokana na Fondoh Che Malone kumsukuma straika Mkongomani wa Prisons, Mambote Batshi na kuzalisha adhabu hiyo iliwapa faida wenyeji.

Kibu tena aliyeisumbua safu ya ulinzi wa Prisons, aliwatoka tena na kuachia shuti la mbali dakika ya 20, lakini lilitoka sentimeta chache na kuwafanya mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani wasiamini macho yao kwa kile kilichotokea.

Ntibazonkiza naye alikosa bao dakika ya 23 akiwa amewekewa mpira akilitazama lango baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', Clatous Chama na Kibu, lakini kwa mshangao wa wengi alipaisha juu.

Nusura Simba ijifunge yenyewe bao dakika ya 32, baada ya beki Malone na kipa wake kujichanganya wakipata presha kutokana na mastraika Jamal Masenga na Jeremiah.

Dakika moja baadaye, Simba ilisawazisha bao dakika ya 33 kupitia kwa Chama aliyefunga kwa mguu wa kushoto akimalizia krosi iliyopigwa na Shomari Kapombe, likiwa ni goli lake la pili msimu huu.

Kama vile haitoshi, Bocco alipachika bao la pili sekunde chache kabla ya mapumziko lililotokana na wachezaji wa Simba kugongeana pembeni ya lango la Prisons na mpira wa mwisho uliingizwa ndani, krosi ndogo na Mzamiru Yassin, ikamkuta mfungaji akausukumiza wavuni, likiwa ni bao lake la kwanza straika huyo msimu huu.

Kipindi cha pili mpira ulichangamka zaidi kuliko dakika 45 za kwanza kwa sababu Prisons hawakukaa tena nyuma, badala yake walikuwa wakipishana na wapinzani wao na kila mmoja akishambulia kutaka kupata bao.

Dakika tano kabla ya mechi kumalizika, Simba ilipata bao la tatu kwa penalti iliyo-

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi afunguka walipokosea

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema sababu kuu ya kuziacha pointi zote tatu ni safu yake ya ulinzi kufanya makosa ambayo wenyeji Ihefu SC waliyatumia vizuri.

Ihefu ilifanikiwa kuifunga tena Yanga mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya na kufikisha pointi sita.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema wapinzani wao walitumia makosa hayo machache huku wachezaji wake wakishindwa kuzitumia vyema nafasi walizozitengeneza na hivyo kulala katika mchezo huo na si kwa sababu ya mwamuzi.

Gamondi alisema licha ya mwamuzi wa mchezo huo kutotenda haki kutokana na baadhi ya maamuzi yake kuwaumiza mabingwa hao watetezi wakati wakielekea kufanya mashambulizi.

"Hali hiyo imekatisha tamaa kwa wachezaji wangu, hatuwezi kuwatupia lawama waamuzi kwa sababu walifanya majukumu yao na wachezaji walishindwa kutumia nafasi walizozitengeneza ili kufunga.

Kumetokea changamoto nyingi katika mechi ya leo (juzi), wengine wamepoteza muda lakini mwamuzi alikuwa na jukumu la kuzuia hayo, hatukuweza kusema tumefungwa kwa ajili ya makosa yake, tunapaswa kuchukuwa lawama za kupoteza mchezo huu," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema alifanya mabadiliko mengi katika mechi hiyo lakini kipindi chote cha kwanza walicheza vizuri na kosa lililofanywa na kipa wao, Djigui Diarra ni la kawaida katika mpira.

Aliongeza wachezaji wake hawakuonyesha kiwango kizuri katika kipindi cha pili hivyo iliwafanya wenyeji kuendelea kutawala mechi hiyo.

"Mechi hii imemalizika, ninawataka wote wasahau matokeo na kujipanga kuelekea

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >